




UKURASA 3

## Tembo alivyoua mzee wa miaka 74 shambani




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 19, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580981

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Utata manispaa upotevu mabilioni



UKURASA 4



CAG Charles Kichere



Waziri wa TAMISEMI, Innocent Bashungwa



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na kuwaaga mahujaji watarajiwa wa Zanzibar, katika Masjid Jamiu Zinjibar Mazizini wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana, watakaoondoka nchini hivi karibuni kuelekea Makka, Saudi Arabia kwa ajili ya kutimiza nguzo ya tano ya Kiislamu kwa ibada ya Hija. **PICHA: IKULU**

# Walichoteta Samia na kigogo wa ACT

UKURASA 2

# Mwinyi aahidi kuja na Mfuko Hijja serikalini

UKURASA 3


**MICHEZO** SIMBA KUANIKA MAJEMBE YOTE UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo (kulia), akipata maelezo kuhusu ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika kijiji cha Lukenge, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro juzi, unaotekelezwa kupitia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo ya Ikolojia Vijijini (EBARR). **PICHA: OMR**

# Walichoteta Samia na kigogo wa ACT

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama Taifa, ACT Wazalendo, Juma Duni Haji, amebainisha mambo matano aliyoteta na Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wa kitaifa hivi karibuni, ikiwamo hali ya kisiasa na kiuchumi.

Kigogo huyo wa ACT Wazalendo aliweka wazi mambo hayo jana katika Kongamano la Tatu la Tume Huru ya Uchaguzi lililofanyika wilayani Songea mkoani Ruvuma.

Katika kongamano hilo, Duni alisema tangu achukue nafasi hiyo ya uenyekiti wa ACT Wazalendo, wamefanya jitihada kuhakikisha chama kinaongoza ajenda ya mabadiliko ya kisiasa kwa kukutana na kufanya mazungumzo na viongozi waandamizi waliopo madarakani na wastaafu.

Alisema kuwa hadi sasa, ameshafanya mazungumzo ya kina na Rais Samia, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Duni alisema katika mazungumzo yake na Rais Samia na Rais Mwinyi, amewaomba kuwa mwaka 2025 uwe mwisho wa utamaduni wa kuingia kwenye uchaguzi unaoacha matukio mabaya, vikiwamo vifo, kisha kutana tena mezani halafu matukio ya namna hiyo kujirudia katika uchaguzi unaofuata.

Kiongozi huyo alisisitiza hoja ya ACT-Wazalendo ya kuwa Tanzania inahitaji Katiba Mpya na mchakato uanze sasa badala ya kusubiri baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 ilivyopendekezwa na kikosi kazi cha Rais Samia.

Pia alisema alimweleza Rais Samia na Rais Dk. Mwinyi kuwa kama ambavyo yeye mwenyewe ameahidi na kuelekeza mara kadhaa, wapate Tume Huru ya Uchaguzi kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

"Ninatilia mkazo ombi la Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kwenye Mkutano wa Kitaifa wa Haki, Amani na Maridhiano kumwomba Rais kupitia vikao vya Bunge vinavyoendelea, Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa ziandikwe upya," alisema.

Duni alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar, bado hali ya maisha ni ngumu kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu.

Alisema katika mazungumzo hayo na viongozi waandamizi serikalini, alisisitiza hoja ya chama chao kuwa ni lazima serikali ichukue hatua za dharura kupunguza bei ya bidhaa muhimu hasa mafuta ya petroli, mafuta ya kula, mbolea na vifaa vya ujenzi.

"Kwenye mazungumzo yangu na Rais Samia, nilimpongeza kwa jitihada anazozichukua kujenga maridhiano na mwafaka wa kitaifa.

"Kwa niaba ya chama changu, ninaomba nichukue fursa hii tena kumpongeza kwa kufungua milango ya mazungumzo na viongozi wa vyama vya siasa na wadau wengine wa demokrasia," Duni alisifu.

Mwenyekiti wa ACT Wazalendo pia alimpongeza Rais Samia kwa ujasiri wa kushiriki majukwaa mawili muhimu aliyoyataja kuwa ni Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ulioitishwa na Baraza la Vyama vya Siasa uliofanyika kwa siku mbili kuanzia Desemba 15 mwaka jana na Mkutano wa Kitaifa wa Haki, Maridhiano na Amani ulioitishwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), ukifanyika kwa siku mbili kuanzia Aprili 5 mwaka huu.

"Tunampongeza Rais Samia kubariki kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Rais cha kuchambua maoni ya wadau kuhusu demokrasia ambacho kinawajibika kwake moja kwa moja.

Ni muhimu Kikosi Kazi kiyafahamu matakwa ya wananchi na kuyalinda na kufungua ukurasa mpya wa kisiasa," alisema.

Aliwaeleza wanachama wake kuwa kama wanavyofahamu, hali ya kisiasa katika kipindi cha utawala wa awamu ya tano haikuwa ya kuridhisha na ilionekana upinzani kufanya siasa ni sawa na uhaini.

Duni alisema ACT Wazalendo pia inamwomba Rais Samia kuzifuta kesi chache za kisiasa zilizosalia mahakamani na kuwaachia huru viongozi wote wa dini waliopo magerezani kwa miaka mingi kwa sababu ya kile ambacho Ofisi ya Mwendesha Mashtaka inasema upelelezi wao haujakamilika.

"Ilikuwa ni miaka sita ya giza kwa demokrasia, mbali na wanasiasa, kila kundi kwenye jamii lilishughulikiwa na kuathiriwa, wakulima, wafugaji, waandishi wa habari, wafanyabiashara, wanafunzi, viongozi wa dini na wanaharakati walipata madhila ya namna mbalimbali katika utawala uliopita," alidai.

Duni alisema Zanzibar wana uzoefu mkubwa wa maridhiano hadi walipofikia Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), kukiwa na makubaliano ya aina hiyo (mwafaka) matatu.

"Kutokana na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Uchaguzi wa Mwaka 2010, tofauti na uchaguzi wowote mwingine uliotangulia, Zanzibar hakukuwa na hata mtu mmoja aliyeuawa.

"Hata Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, kabla ya matokeo kufutwa, uchaguzi ulikwenda vizuri na mgombea wa upinzani, Seif Sharif Hamad alikuwa amefanya vizuri.

Maridhiano yanajenga mwafaka wa kitaifa, umoja na mshikamano katika taifa," alisema.

Alitaja uzoefu mwingine kutoka Zanzibar kuwa ni athari za kupuuzwa kwa makubaliano yanayowekwa.

Alisema siyo jambo linalofaa kwamba sehemu kubwa ya makubaliano ambayo yamekuwa yakifanyika kila baada ya uchaguzi hayatekelezwi.

Kiongozi huyo aliendelea kusisitiza hoja ya ACT Wazalendo kuhusu umuhimu wa Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kuyafanyia kazi makubaliano yake na Maalim Seif Hamad kabla ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya sasa.

Pia alisema ACT Wazalendo inasisitiza umuhimu wa kuwa na mageuzi ya kisheria na kupendekeza mabadiliko kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria na Kanuni zinazoongoza Jeshi la Polisi ili uwanja wa kisiasa uwe huru kwa mujibu wa sheria na siyo huruma ya watawala.

## Viwanda vyaagizwa kutenga fungu utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) amewataka wamiliki wa viwanda kutenga fungu kwa ajili ya shughuli za kimazingira.

Khamis Hamza Khamis alitoa rai hiyo jana alipofanya ziara ya kikazi ya kujionea uzingatiaji wa sheria ya mazingira katika kiwanda cha kuzalisha mafuta ya alizeti cha Pyxus kilichoko eneo la Kizota jijini Dodoma.

Alisema mataifa mbalimbali yaliyoendelea hutoa fedha kwa nchi zinazoendelea kwa kutambua kuwa wao ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira kutokana na hewa ya ukaa wanayozalisha.

Naibu waziri huyo alisema viwanda havina budi kuchangia shughuli za mazingira na za kijamii kwa ujumla zikiwamo upandaji miti, utoaji elimu kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Ninawapongeza kiwanda hiki cha Pyxus nimesikia mnafanya shughuli za kupanda miti katika eneo lenu, hivyo ninatoa wito kwa viwanda vingine nchini viwe na utaratibu huu ili tuhakikishe tunatunza mazingira," aliagiza.

Aliwataka wamiliki wa viwanda vyote nchini wawe na mfumo mzuri wa kutibu na kudhibiti majitaka ili kuhakikisha hayatiririki na kumwagika kwenye makazi ya watu, hali inayoweza kuhatarisha afya na mazingira.

Pia alielekeza viwanda vidhibiti moshi unaotokana na shughuli za viwandani usisambae katika makazi ya watu, hali inayoweza kuwasababishia matatizo ya kiafya. Vilevile, alielekeza viwanda vidhibiti kelele zinazotokana na mashine za viwandani zisiwe kero kwa wananchi kwa kuwa zinaweza kuwasababishia matatizo ya masikio.

Meneja Rasilimaliwatu wa Kiwanda cha Pyxus, Gideon Mutta, alisema uongozi wa kiwanda hicho umepokea maelekezo hayo na kuahidi yatashughulikiwa.

Hata hivyo, meneja huyo alisema wanakabiliwa na shida ya miundombinu ya mfumo wa majitaka, akiiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) kuwasaidia na kuona namna ya kuwaunganisha na mfumo wa Jiji la Dodoma.

HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea taarifa ya utekelezaji wa operesheni ya anwani za makazi kutoka kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# Tembo aua mzee wa miaka 74

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

MZEE mwenye umri wa miaka 74, Nyeusi Maghiya, mkazi wa Kitongoji cha Kakamega, Kijiji cha Mlumbi, Kata ya Mang'onyi wilayani Ikungi mkoani Singida, ameuawa kwa kukanyangwa na tembo wakati akivuna mtama shambani.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, ambaye alifika katika kijiji hicho haraka baada ya kupewa taarifa, alisema tukio hilo limetokea jana majira ya saa tatu asubuhi baada ya tembo watatu kuvamia katika kitongoji hicho na kisha kumkanyaga mzee huyo na kumvunja miguu,mikono na mbavu na kusababisha umauti.

Tukio hilo ni la pili kutokea katika kata hiyo mwaka huu ambapo wiki tatu zilizopita, tembo alimuua mtoto mwenye umri wa miaka mitatu katika Kijiji cha Ituntu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mlumbi, Issa Abdalla, na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kakamega, walimweleza Mkuu wa Wilaya kuwa tembo wamekuwa wakipita mara kadhaa katika kijiji vya Kata ya Mang'onyi na kusababisha vifo na uharibifu mkubwa wa mazao shambani.

Walisema kutokana na hali hiyo, wananchi wamekuwa na hofu na wanafunzi kuogopa hata kwenda shuleni kwa hofu ya kushambuliwa na tembo ambao wameendelea kuwa tishio katika kata hiyo.

Wenyeviti hao waliiomba serikali kufanya haraka utaratibu wa kuwaondoa tembo hao ili wananchi wawe na amani na kuendelea na shughuli zao za uzalisha hususani katika kipindi hiki ambacho ni cha mavuno mashambani.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Muro, akizungumza na wananchi katika eneo la tukio, alisema serikali imeandaa programu ya kuyatambua maeneo ambayo yamekuwa sugu kwa mwingiliano wa wanyama kupita ili kuhakikisha wanaondolewa, ili wasiendelee kuleta madhara zaidi.

"Wilaya yetu imekumbwa sana na changamoto hii ya tembo na tumeshatoa taarifa kwa wenzetu wa maliasili ambapo wiki tatu zilizopita tembo aliua mtoto wa miaka mitatu na leo (jana) tumepata msiba wa mzee wetu kuuawa na tembo, tumeshatoa taarifa waondolewe," alisema.

Muro aliwaomba wananchi wakiona tembo, wasianze kuwakimbiza na kuwashambulia kwani wamekuwa wakipita tu na tembo anapoona anashambuliwa, anajihami na kuanza kushambulia.

"Ombi langu kwenu wakati serikali inaendelea kupambana na changamoto hii, wananchi mchukue tahadhari ya maisha yenu. Unapoona tembo, rudi nyumbani, chukua watoto wako mnajifungia ndani na mtatoka nje mtakapoelezwa na viongozi wenu wa kijiji au kitongoji kama tembo wameshaondoka," alielekeza.

Alisema wananchi wasijaribu kuwashambulia au kuwakimbiza kwa kuwa hawana utalaamu na wanyama hao kwa kuwa kipindi hiki cha mavuno, kimekuwa na idadi kubwa ya wanyama kama tembo kupita.

Muro pia aliwataka wananchi wawe wanatunza vyakula ndani ya nyumbani kwani wanyama wanaposikia harufu ya chakula, hufika kwenye makazi ya watu kutafuta chakula.

Kata za Mang'onyi na Ntuntu tembo wamekuwa wakipita mara kwa mara na katika historia inaonyesha maeneo hayo ni ushoroba ambao walikuwa wakipita miaka ya zamani kabla watu hawajaongezeka na kuweka makazi kwenye maeneo hayo ya ushoroba wa tembo.

## Majaliwa aagiza utatuzi migogoro matumizi ya ardhi anuani na makazi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitaka taasisi zote zenye dhamana ya masuala ya ardhi na makazi kuhakikisha zinakuja na mikakati thabiti ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi iliyoainishwa wakati wa utekelezaji wa zoezi la operesheni ya anuani na makazi.

Kiongozi huyo alitoa agizo hilo jana wakati akipokea taarifa ya utekelezaji wa mchakato wa operesheni ya anuani na makazi kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Majaliwa aliwataka watoe miongozo ya namna bora ya kushughulikia matatizo ya Watanzania ya kuishi katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria ili kuhakikisha watu wote wananufaika na fursa zitokanazo na mchakato huo.

Pia aliwataka viongozi katika ngazi zote hususani kwenye Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha wanasimamia kikamilifu utunzaji wa mifumo sambamba na kulinda miundombinu ya anwani za makazi kwenye maeneo yao.

"Viongozi na watendaji hakikisheni kuwa jamii inaendelea kuelimishwa ili kujua manufaa sanjari na kutumia fursa zitokanazo na uwapo wa anwani za makazi katika maeneo yao," alisema.

Majaliwa aliziagiza wizara zote, sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kushughulikia matatizo yote yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa operesheni anwani za makazi na kuhakikisha mchakato huo unakuwa endelevu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleimani Abdulla, alisema ni matarajio ya Watanzania kuwa kukamilika kwa Operesheni ya Anuani na Makazi kutasaidia kuongeza uwezekano wa kuendelea kukuza uchumi kuwa kidijitali.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema hadi kufikia Mei 31 mwaka huu, kupitia operesheni hiyo, taarifa na anuani za makazi 12,385,956 zilikusanywa, sawa asilimia 106.94 ya lengo lililokusudiwa.

Alisema hilo ni zaidi ya lengo walilojiwekea awali la kukusanya taarifa na kutoa anuani za makazi 11,582,106.

# Rais Mwinyi aahidi kuja na Mfuko wa Hijja kuwasaidia wasio na uwezo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali anayoiongoza, itahakikisha inatengeneza Mfuko wa Hijja ili kuwasaidia wasio na uwezo wa kwenda kufanya ibada ya Hijja, kupata fursa hiyo.

Dk. Mwinyi alieleza hayo jana wakati akiwaaga mahujaji watarajiwa wa Zanzibar wanaokwenda kutekeleza ibada ya Hijja huko Makka, Saud Arabia mwaka huu, hafla iliyofanyika huko Masjid Jamii Zanjibar, Mazizini Mkoa wa Mjini Magharibi. Alisema Mfuko wa Hijja utawasadia kwa kiasi kikubwa wale ambao hawana uwezo wa kwenda kutekeleza ibada hiyo huko Makka sambamba na kufikia lengo na madhumuni ya kupata watu wengi kwenda Hijja. Aliwaomba waumini kuwa na subira kutokana na kuwapo kwa masharti ya umri katika ibada ya Hijja ya mwaka huu huku akipongeza idadi ya mahujaji waliojitokeza mwaka huu kwenda kutekeleza ibada hiyo licha ya vikwazo vilivyojitokeza.

Akitoa ufafanuzi kuhusu maombi ya mahujaji kwa serikali, alisema kuwa kwa upande wa huduma ya vipimo vya PCR, hivi sasa huduma hiyo inatolewa na sekta binafsi kwa dola 80 ambapo katika makubaliano na serikali dola 50 inakwenda kwa serikali na dola 30 inakwenda kwa sekta binafsi na kueleza utayari wa serikali kuondoa dola 50 na kubakisha ya watoa vipimo hao huku akihidi kuwaomba ili kinachotolewa na mahujaji kiwe kidogo zaidi.

Rais huyo alisema serikali itatazama uwezekano wa kuondosha cheti cha afya kama ilivyo kwa Tanzania Bara huku akieleza kwamba amelipokea suala la akaunti maalum ya Zanzibar kwa ajili ya Hijja na kueleza kwamba suala hilo litafikishwa katika ngazi husika ili kuondoshwa kwa kuwa limefikia pazuri. Alieleza kuna kazi ya ziada ya kufanywa na serikali, taasisi pamoja na wananchi kwa ujumla ya kujifunza hasa kwa nchi zenye Waislamu wengi kama vile Malaysia na Indonesia ambapo huanza mipango ya kwenda Hijja mapema.

Dk. Mwinyi alisema miongoni mwa mipango inayofanywa na nchi hizo, ni pamoja na utaratibu mzuri wa kukukusanya fedha za Hijja kwa sababu kuna wazazi wanaaza kuwawekeza watoto wao akauti za Hijja mara tu anapozaliwa mtoto mpaka pale anapofikia umri wa kwenda kuhiji fedha zinakuwa tayari zimeshakamilika.

Alhaj Dk. Mwinyi alisisitiza suala la umoja na kueleza haja ya kuendeleza umoja wao hasa kwa mahujaji hao wakati wakiwa katika ibada hiyo ya Hijja huko Makka, Saud Arabia. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kufuatilia kwa karibu safari ya Hijja ya mahujaji wa Znz.

Alisisitiza haja ya kuiombea dua nchi pamoja na kumwombea dua Rais Dk. Mwinyi ili azidi kuiletea maendeleo Zanzibar huku akisisitiza suala zima la Hijja kwa mahujaji na kufuata maelekezo ya viongozi.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, aliwaeleza mahujaji hao umuhimu wa Hijja na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu kukubaliwa Hijja zao.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Sheikh Abdalla Talib, alisema maandalizi ya Hijja yakikamilika hukutana na usiku wa siku ya pili viongozi wa taasisi za Hijja huenda Saudia Arabia na kwa mwaka huu Juni 22 kundi la kwanza linatarajiwa kuondoka kuelekea Saud Arabia.

Alisema kuwa Zanzibar imeanza utaratibu wa kuratibu shughuli za Hijja tangu mwaka 1923, wakati huo ilikuwa ikiratibu kanda yote ya Afrika Mashariki. Mnamo mwaka 1945, kwa mara ya kwanza watu walitakiwa wachukue pasi za kusafiria pamoja na mahujaji kuanza kwenda kwa usafiri wa ndege ambapo kundi la kwanza kusafiri kwa Afrika Mashiriki lilitokea Zanzibar.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hijja, Yussuf Salim Yussuf, akisoma risala ya Umoja wa Taasisi za Hijja Zanzibar (UTAWAZA), alisema kwa mwaka huu wanaziratibu taasisi 23 zinazotegemea kusafirisha mahujaji 1,600 huku akieleza lengo la taasisi hiyo ni kuimarisha huduma za Hijja na kuzifanya ziwe na ufanisi zaidi.

# LHRC: Bajeti pendekezwa nzuri, lakini...

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimepongeza mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23 kwa kulenga kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi, huku kikikosoa baadhi ya maeneo katika bajeti hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam juzi kuhusu uchambuzi wa bajeti pendekezwa hiyo kwa mtazamo wa haki za binadamu, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema imezingatia mambo muhimu.

"Kwa mfano, kilimo kimekuwa kikifanyika katika mazingira duni yenye matokeo yasiyotabirika, serikali imependekeza kuongezeka bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 294 za mwaka wa fedha wa 2021/22 hadi kufikia Sh. bilioni 954 kwa mwaka wa fedha wa 2022/23," alisema.

Alisema serikali imepanga kuongeza idadi ya maeneo ya kilimo yenye miundombinu ya uhakika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kwamba hilo litafanyika kwa kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta milioni 8.5 ambazo zinategemewa kupunguza tatizo la umaskini kwa vijana na wanawake.

"Tunaipongeza serikali kwa hilo kwani hatua hiyo inakwenda kuboresha miundombinu ya kilimo cha kisasa. Iwapo mpango huo utafanikiwa, maisha ya wazalishaji wadogo hasa wa vijijini, wakiwamo wanawake na vijana, yanaweza kuwa bora kwa kuongeza kipato," alisema.

Anna alisema hatua hiyo itachochea kasi ya maendeleo na kuongeza pato la wananchi kupitia kilimo, lakini pia akagusia suala la mapendekezo ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa nchini.

"Hatua hizi za kibajeti zinatarajiwa kuleta matokeo chanya katika maeneo mawili, kwanza kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo na upatikanaji uliowezeshwa wa pembejeo," alisema.

"Kwenye elimu, Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema, kitendo cha serikali kuondoa ada kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha sita kinalenga kusaidia wanafunzi wanaotoka katika familia maskini.

"Bajeti imeelekeza kuanzisha dirisha maalum lililopangiwa Sh. bilioni nane kupitia TASAF, litakalosaidia watoto hao ikiwa ni pamoja na kudhibiti mimba za utotoni, kwani mabweni ya wasichana yataongezeka," alisema.

Alisema kituo hicho kinaipongeza serikali kwa hatua zote ambazo inachukua kwa manufaa ya Watanzania, ikiwamo kupunguza matumizi ya serikali kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA kama njia ya mawasiliano serikalini.

"Hotuba ya bajeti imekemea tabia ya matumizi mabaya ya magari ya serikali kwa safari za binafsi na za kikazi zisizo na tija, ikiwamo mtumishi kusafiri kwa ndege huku gari likitangulia kwa ajili ya mapokezi aendako," alisema.

Alisema pamoja na kutoa pongezi, kituo hicho kimeona upungufu kwenye bajeti hiyo likiwamo suala la bima ya afya kwa wote, kwamba serikali imekuwa ikihimiza umuhimu bima hiyo lakini kwenye bajeti haikutajwa.

"Pamoja na mazuri tulioainisha, tumebaini maeneo kadhaa yenye changamoto ikiwamo bima ya afya kwa wote. Tunapendekeza serikali na Bunge kuzingatia hitaji la kutenga bajeti kwa ajili ya bima ya afya kwa wote," alisema.

Upungufu mwingine ulioainishwa katika bajeti hiyo ni kupendekeza kushushwa kwa asilimia ya mikopo kwa ajili ya makundi maalumu kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, serikali ikipendekeza sasa iwe mbili kwa wanawake na vijana na asilimia moja kwa watu wenye ulemavu.



Wakazi wa Kumburu Estate, kata ya Ngomeni, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa kwenye foleni ya kuchota maji katika mradi wa maji uliotekelezwa na Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Utata manispaa upotevu mabilioni

**Na Waandishi Wetu**

JULAI 2016, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iligawanywa na hivyo kuzaliwa Halmashauri mbili za Manispaa ya Ubungo na Kinondoni.

Baada ya mgawanyo huo, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilipata mgawo wa vyumba saba vya kupangisha vilivyoko Oysterbay Villa, Mitaa ya Mawenzi na Ruvu.

Hata hivyo, imebainika kuwa tangu kufanyika kwa mgawanyo huo, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo haikuwahi kukusanya kodi ya pango katika vyumba hivyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu kuanzia mwaka 2017/18, hivyo kupoteza mapato ya Sh. milioni 720.

Shida ni nini? Nipashe ilifika kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo mwanzoni mwa wiki na kuzungumza na Ofisa Biashara wa Manispaa ya Ubungo, Prisca Mjema, aliyesema kuwa kuna sababu tatu zilizochangia halmashauri kutokusanya kiasi hicho cha fedha ikiwamo kuchelewa kukabidhiwa miradi hiyo na Manispaa ya Kinondoni.

Alisema kuwa licha ya halmashauri hizo kugawanywa mwaka 2016, walikabidhiwa rasmi miradi hiyo mwaka 2019, hivyo kipindi chote cha takriban miaka mitatu hawakunufaika na miradi hiyo.

"Mchakato wa kugawana mali na madeni huwa unachukua muda kwa kuwa ni vitu ambavyo vinaenda kwa utaratibu. Kwa hiyo, kwenye hizi nyumba za Oysterbay tulikabidhiwa rasmi kutoka Manispaa ya Kinondoni Aprili 12, 2019 kwamba na sisi sasa tunamiliki 'apartment' saba," Prisca alisema.

Alitaja sababu nyingine ni kuchelewa kwa mzabuni kupata wapangaji, akifafanua kuwa baada ya kukabidhiwa nyumba hizo, walitafuta mzabuni wa kuzipangisha ili ziingize mapato na kufanikiwa kumpata mwezi Novemba, 2019 lakini naye alikaa mwaka mzima bila kupata mpangaji.

"Mwaka mzima walikaa bila kupata mteja kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo corona (UVIKO-19) na kudorora kwa uchumi. Kwa hiyo, wageni walikuwa hawaji nchini, hivyo kukawa na hiyo changamoto.

"Tulivyoona mwaka mzima hakuna wapangaji, tukasitisha mkataba na huyo mzabuni," Prisca alisema na kubainisha kuwa Februari 2021, walipata mzabuni mwingine ambaye alipata wapangaji wa kuishi kwenye nyumba nne za Mtaa wa Mawenzi kwa kodi ya dola 1,250 (Sh. 2,913,750) kwa mwezi kwa kila nyumba ambapo mpaka Machi 2022, walikuwa wamekusanya takriban Sh. milioni 100 kutoka kwenye nyumba hizo.

**SHIDA MTAA WA RUVU**

Ofisa huyo alidai lipo tatizo katika nyumba zao zilizoko Mtaa wa Ruvu kutokana na mwekezaji waliyeingia naye mkataba kuwa na kile alichokiita kukatisha tamaa wateja.

"Ni matarajio yetu kuwa Manispaa ya Kinondoni ambayo pia ina nyumba zake huko, itaweka mambo sawa na mwekezaji huyo kwa sababu sasa hivi nchi imefunguka na watu wanataka kupanga nyumba na serikali pia inahitaji kuingiza mapato," alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Mweka Hazina wa Manispaa hiyo, Onesmo Monga, alisema wamepiga hatua zaidi katika kutafuta ufumbuzi wa suala hilo, ikiwamo kufungua kesi mahakamani ili kumaliza matatizo ya kisheria yaliyoibuka kati yao na baadhi ya wapangaji.

**JICHO LA CAG**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hayuko mbali na upotevu wa mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo.

Mbali na kuangazia upotevu wa Sh. milioni 720 kutokana na kutokusanya mapato kwenye nyumba hizo za mgawanyo wa Manispaa ya Kinondoni, CAG Charles Kichere, katika ripoti yake kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni miezi miwili iliyopita, alibaini Manispaa ya Ubungo imepoteza jumla ya Sh. bilioni 4.64 kutokana na usimamizi dhaifu wa ukusanyaji wa mapato.

CAG Kichere anasema alifanya ukaguzi maalumu wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/2021 na kubaini upungufu katika ukusanyaji wa mapato na kusababisha hasara hiyo ya Sh. bilioni 4.64.

Ukiachilia mbali Sh. milioni 720 za nyumba hizo za mgawo, CAG anasema alibaini kuwapo kwa maeneo ya wazi yenye ukubwa wa mita za mraba 69,020 yaliyokuwa yamevamiwa ambayo yengeweza kuiingizia halmashauri hiyo Sh. bilioni 2.96 endapo yangekuwa yamepangishwa kwa kutoza Sh. 15,552 kwa mita moja ya mraba kama ilivyokuwa imeazimiwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha cha Februari 12, 2019.

"Katika zabuni Na. LGA/180/2018-2019/NCS/53 LOT 2 na LGA/180/2018-2019/NCS/53 LOT 1 ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada za choo katika Kituo cha Mabasi cha Simu 2000 na Soko la Mabibo, halmashauri ilitunuku zabuni kwa mawakala walionukuu kiasi cha chini cha mapato Sh. milioni 131.96 na kuwaacha wa kiasi cha juu Sh. milioni 207, hivyo kusababisha upotevu wa Sh. milioni 75.04 bila sababu za msingi.

"Vilevile, nimebaini halmashauri imepoteza mapato ya Sh. milioni 373.39 katika ushuru wa vibanda na vizimba vilivyopo katika masoko ya halmashauri kutokana na kukusanya ushuru kwa kutumia viwango vya chini vya Sh. 500 kwa siku kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo Na. 226 ya tarehe 22 Machi 2019.

"Nimebaini kuwa halmashauri inadai ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara 38 wakubwa kati ya biashara 6,270 na kuikosesha halmashauri mapato ya Sh. milioni 507.52 kinyume cha Kifungu cha 6(1) (u) na 7(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019)," anafafanua.

CAG pia anasema amebaini hasara ya Sh. milioni 284.31 iliyotokana na kutokatwa kwa asilimia 10 ya kazi zilizosalia wakati wa kusitisha mkataba wa ujenzi wa jengo la utawala.

Anafafanua kuwa mnamo Juni 23, 2020, halmashauri ilisitisha mkataba wa ujenzi wa jengo la utawala na mkandarasi kutokana na ukiukwaji wa masharti ya mkataba uliofanywa na mkandarasi.

"Nimebaini halmashauri haikumkata mkandarasi kiasi cha Sh. milioni 384.31 ikiwa ni tozo ya asilimia 10 ya kazi zilizosalia zenye thamani ya Sh. bilioni 2.84 kinyume cha kipengele cha 68.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba namba LGA/180/2017-2018/W/11 wenye thamani ya Sh. bilioni 6.3," anabainisha.

Katika mapendekezo yake, CAG anasema kuna haja Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam wakishirikiane na mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki waliotajwa katika taarifa maalum kwa kuisababishia halmashauri hasara kutokana na kutofuata sheria na taratibu na vipengele vya mkataba.

CAG pia anapendekeza mawasiliano yafanyike kumpata mkandarasi ili kuhakikisha kuwa Sh. milioni 284.31 zinarejeshwa kwa halmashauri.

**■Imeandaliwa na Jenifer Gilla, Sechellar Necter na Haika Christopher (SJMC)**

# Wizara yazindua vifaa matengenezo ya ndege

**Na Grace Gurisha**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imezindua vifaa vitatu vya uhandisi wa matengenezo ya ndege vinavyogharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa ajili ya kuzalisha wataalamu wenye weledi mkubwa.

Vifaa hivyo vilizinduliwa jana chuoni huko na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo, ambaye alisema kupitia mradi wa kukuza ujuzi ambao upo kwenye nchi kama tatu za Afika Mashariki, umepata fedha kutoka Benki ya Dunia (WB) na kuvinunua.

Aliahidi kuwa vifaa hivyo vitatumika vizuri kuwapa ujuzi wahandisi wanaohusika kutengeneza ndege, ambapo wataweza kufanya kazi za mikono kwa sababu anapofundishwa lazima ashike chombo.

Prof. Nombo alisema mhandisi anapotoka katika chuo hicho, akienda kwenye karakana ya ndege moja kwa moja anaweza kufanya matengenezo yanayotakiwa kwa sababu alipokuwa kwenye mafunzo alitumia vifaa.

"Kama mnavyojua nchi yetu ina ndege nyingi na itaendelea kuongeza nyingine, kwa hiyo tunahitaji kuwa na wahandisi wenye uwezo wa kuhudumia ndege kwenye matengenezo na kutoa huduma zenye ubora," alisema.

Naibu huyo alitoa wito kwa wakufunzi kutumia vifaa hivyo kwa malengo yanayotarajiwa na kueleza kuwa anaamini watawapa maelekezo mazuri na halisi wanafunzi katika kuvitumia vifaa.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, alivitaja vifaa hivyo kuwa ni kompyuta za kisasa ambazo zinatumika kufundishia wahandisi wa ndege duniani.

Alisema vifaa vingine ni VMT ambavyo vinatumika Marekani na Air bus ya nchini Ufaransa.

"Amezindua injini mbili za ndege ndogo zinazotumiwa na TANAPA, uwanja wa ndege Terminal one na kule Arusha na Zanzibar hizo ndege zinatumia piston injini na zinatumia mafuta kama ya taa," alisema.

Alisema wana injini ya Jet ambayo inatumika kwenye ndege za kisasa kama Air bus au Dreamliner ambayo inatumia mafuta aina ya 'Jet Fuel'.

Kuhusiana na gharama za vifaa hivyo, Prof. Mganilwa alisema hana takwimu sahihi lakini vifaa vya VMT vimegharimu Dola za Marekani 250,000 na injini zimegharimu Dola 350,000.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kulia), akimsalimia mtoto mwenye ulemavu, Angerina Aloyce, wakati wa maadhimisho ya Mtoto Mwenye Ulemavu kuelekea Kilele cha maadhimisho ya Mtoto wa Afrika, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, iliyoambatana na harambee ya kuchangisha pesa za kuwakatia bima za afya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ACT: Wananchi walipwe fidia kabla ya ubomoaji

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeitaka serikali kusitisha mpango wa kuvunja Soko la Manzese B lililoko Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma hadi wafanyabiashara wa soko hilo wataposhirikishwa vya kutosha na kulipwa fidia.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, alipokwenda sokoni huko na kufanya kikao na wafanyabiashara wa soko hilo.

"Nimeambiwa serikali inataka kuvunja soko hili na kujenga soko jipya la kisasa. Hatua hiyo ni njema, lakini ninafahamu soko hili lilijengwa na ninyi wafanyabiashara na mkataba wenu na halmashauri unamalizika mwaka 2025.

"Hivyo basi, si haki kwa serikali kutaka kulivunja kabla ya kuzungumza na ninyi na kuwalipa fidia. Nimeelezwa kuwa mmepewa notisi ya kuhama ifikapo tarehe Mosi Julai, 2022.

"Ninamuomba Waziri Mwenye dhamana ya TAMISEMI, Ndugu Innocent Bashungwa kuingilia suala hili. Mradi huu hauwezi kutekelezwa kabla ya kuwalipa fidia wafanyabiashara na kuwatafutia maeneo mazuri ya kwenda.

"Pia, mradi ukikamilika, wafanyabiashara wa sasa wapewe kipaumbele kupewa maeneo," Katibu Mkuu huyo alifafanua.

Alitoa rai kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwamulika wawakilishi wake wa ngazi za chini kwa kuwa baadhi ya uamuzi wao unawaumiza wananchi maskini na hivyo kuipaka matope serikali.

"Soko hili lina wafanyabiashara 700. Unapowaumiza watu 700, unakuwa umeumiza maelfu ya familia zao na kuwajengea chuki na serikali," alionya.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu huyo wa ACT Wazalendo amemtaka Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha serikali za vijiji zinazingatia taratibu za uuzaji wa ardhi ya kijiji.

Alitoa rai hiyo juzi alipotembelea Kijiji cha Kipingo kilichoko Jimbo la Madaba, wananchi wa kijiji hicho wakilalamika kuhusu kitendo cha Serikali ya Kijiji kuuza zaidi ya ekari 1,500 za kijiji bila baraka za Mkutano Mkuu wa Kijiji.

Wanakijiji hao walidai kuwa wale ambao wamekuwa wakihoji dhidi ya suala hilo, wanakamatwa na Jeshi la Polisi, kupigwa na kubambikwa kesi. Aliwaahidi wanakijiji hao kuwa ACT Wazalendo kupitia Kamati ya Kuisimamia Serikali ya Wasemaji wa Kisekta, itafuatilia suala hilo.


STEP MARK

Makumbusho, PLOT No. 13 Block 45, P.O.Box 11767, Dar es salaam, Tanzania
Office : +255 715 300 312 , E-mail: info@stepmark.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA!!

**Step mark Limited** kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya CRDB Makao Makuu** yaliopo **Plot Namba. 25&26 Ally Hassan Mwinyi Road & Plot Namba.21.Barack Obama Road, S.L.P 268,11101 Dar es Salaam** tunatangaza minada ya hadhara wa kuuza mali za wadaiwa wa **Benki ya CRDB** sehemu mbali mbali katika mikoa ya Tanzania.

Mali hizo zitauzwa kama zilivyo kwenye eneo kwa njia ya Minada ya hadhara..

| S/No | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI | TAARIFA YA MALI INAYOUZWA | ENEO MALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Israel Delius Mahenge | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa: Mwanyanje Kata: Igawilo Jiji la Mbeya. | 03/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 2. | Joshia Daniel Magabe | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa; Mponja Kata;Igawilo Jiji la Mbeya | 04/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 3. | Gasper Johnson kiando | NYUMBA | Hati namba 89-RUKLR Namba ya makazi 791609 | Ploti namba 383 Block 'T' Mtaa;kisiwani Sumbawanga | 04/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 4. | Apolinary Sipriano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 5. | Apolinary Sipriano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 6. | Apolinary Sipriano Selemani | GARI | Namba ya usajili. T926DBZ Chassis No: MAT382042E7R11237 Aina: LP Aina ya Umbo:BUS Usajili wa kadi: 7812249 | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 7. | Masiwa hardware Supplies limited | GARI | Namba ya usajili. T777DJJ Chassis No:IXGTT10ACGA000604 Aina: TT100A Aina ya Umbo: Trailer Usajili wa kadi: 7658635 | Sumbawanga | 9/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 8. | Bakari Said Mayongo | NYUMBA | Hati namba; 25302-MBYLR Namba ya makazi;381142 | Ploti namba 237, Block 'OO'high dendity Sumbawanga | 12/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 9. | Venus Joseph Ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; sheli Kata; Nchola Wilaya; Namanyere Mkoa;Sumbawanga | 15/07/ 2022 Saa Nne Asubui Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 10. | Venus joseph ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; minsukumilo Kata;kipindu Wilaya; namanyere Mkoa;sumbawanga | 16/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 11. | Friday Samson mziho | NYUMBA | Hati namba; 48063 MBYLR, Namba ya makazi;991835 | Ploti namba 1, Block 'A'medium dendity majengo, Namanyere urban area. | 18/07/ 2022 Saa Nne Asubui Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 12. | Paul Phares Mnyandwa | NYUMBA | Hati namba; 2124 Namba ya makazi;1031860 | Ploti namba 413, Block 'V' Unguu Road GAIRO. | 19/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni. |
| 13. | Sawaka Nchola Ganja | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; matai B Kata; Nchola Wilaya; | 20/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi lazima afike eneo la mnada unapofanyika
2. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano(25%) ya bei iliofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada na mteja akishindwa kulipa 75% ndani ya siku 14 atakua amepoteza haki ya ununuzi.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA**
**0677 992 040 /0677 992 030**

2169908702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matumizi ya fedha Mamlaka Serikali za Mitaa yamulikwe

**UNAPOZUNGUMZIA** matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, moja kwa moja unagusa fedha za makusanyo ya mapato ya ndani, fedha kutoka Serikali Kuu, wahisani na michango ya wananchi.

Baadhi ya vyanzo vya fedha hizo ni Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG), Ruzuku ya Maendeleo ya Sekta ya Afya (HSCDG), Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), Malipo ya Matokeo (EP4R) na Mpango wa Kuboresha Ubora wa Elimu (EQUIP-T).

Pia unazigusa fedha za miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mfuko wa Afya ya Jamii, Mradi wa Uimarishaji wa Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Wakati kukiwa na miradi mingi katika mamlaka hizo, tayari kuna angalizo la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu matumizi ya fedha katika mamlaka hizo, akipendekeza hatua zichukuliwe haraka kudhibiti dosari zilizoko huko.

Tathmini ya utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo iliyofanywa na CAG kwa mwaka 2020/21, inaonesha kuwapo dosari nyingi.

Mathalani, CAG kupitia tathmini ya matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, alibaini fedha zisizotumika zilikuwa kati ya asilimia 53 na 76, sawa na wastani wa asilimia 41 ya fedha zilizokuwapo kutokana na vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hiyo ni ishara kuwapo shida ya kutotumia fedha zilizopangwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hivyo kuziweka fedha hizo katika hatari ya kubadilishiwa matumizi na kutekeleza shughuli zingine ambazo awali hazikupangwa.

CAG pia alibaini halmashauri 185 zilikuwa na miradi ambayo haikutekelezwa; miradi iliyokamilika lakini haijaanza kutumika; miradi iliyoko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na miradi ambayo fedha zake zilielekezwa katika shughuli zisizokusudiwa.

Lipo tatizo katika matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, CAG katika kipindi tajwa, akibaini miradi ya mamilioni ya shilingi imetekelezwa kinyume cha matakwa ya sheria katika Halmashauri za Miji ya Korogwe na Singida, pia wilaya za Kyela, Biharamulo, Butiama, Bumbuli, Karatu, Pangani na Longido.

Dosari hizo zinajumuisha fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kutumika kufadhili miradi ya taasisi za kisiasa na kidini, ambayo haikuwa na manufaa mapana ya jamii kinyume cha matakwa ya sheria iliyoanzisha mfuko huo.


Katika hili, Nipashe tunakumbusha umuhimu wa kamati husika na mfuko huo na serikali kwa ujumla, kuzingatia masharti ya Sheria ya Mfuko katika kuidhinisha na kuhamishia fedha kwenye miradi inayoanzishwa na jamii.

Kama hakutakuwa na udhibiti wa matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni wazi kuwa kiasi kikubwa cha fedha kinachoelekezwa kwenye mamlaka hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kitatumika vibaya kama ilivyoshuhudiwa kwenye maeneo tajwa.

Tunaona ipo haja kuchukua hatua kudhibitiwa matumizi mabaya ya fedha za mamlaka hizo kwa kuhakikisha kunakuwapo ufuatiliaji wa karibu ili fedha zitumike kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vijana wasishinde mitandaoni, wajiandae kuwa taifa lililo bora

Na Sabato Kasika

**VIJANA** ni taifa la kesho wanaotakiwa kujengwa katika misingi ya kuwafanya wawe viongozi bora wa baadaye, pia wazee wenye busara wa baadaye watakaotegemewa na taifa kwa ushauri.

Ushiriki na mchango wao vinahitajika katika uhai wa taifa, lakini kinyume cha hapo, nchi inaweza kukosa viongozi makini wa baadaye na kuwa na wazee wa baadaye wasio na manufaa kwa nchi yao.

Kwa kulitambua hilo, ni muhimu kuandaa mazingira rafiki kwa vijana ili washiriki katika masuala ya kisiasa kwa kuwa siasa ni miongoni mwa majukwaa yanayoandaa viongozi wa baadaye.

Hata hivyo, vijana wanapoandaliwa kuwa viongozi, si lazima wawe wa kisiasa, bali wanaweza kuongoza taasisi mbalimbali zikiwamo za umma na hata kwenye jamii inayowazunguka.

Kimsingi, vijana wanatakiwa kuchangia katika maendeleo ya nchi yao, lakini hali ilivyo, inaonyesha huenda wakakosekana viongozi wa baadaye na kupata wazee ambao itakuwa vigumu kuchota busara kwao.

Kwa nini? Baadhi ya vijana hawajui kinachoendelea katika nchi yao, hawatoi maoni na hata linapotokea jambo ambalo wanatakiwa kutoa maoni, imekuwa kawaida kwao kukaa kimya.

**Kwa nini? Baadhi ya vijana hawajui kinachoendelea katika nchi yao, hawatoi maoni na hata linapotokea jambo ambalo wanatakiwa kutoa maoni, imekuwa kawaida kwao kukaa kimya.**

Kundi hilo ndilo ambalo sasa linashuhudiwa likishinda kwenye mitandao ya kijamii kuandika mambo ambayo hayana umuhimu na pia wanafuatilia mambo yasiyo na maana kwao, pia kwa taifa lao.

Ndiyo hao hao ambao wanaoishi kwa kutegemea wanasiasa wakiwatumia kufanikisha mambo yao huku wakiona kama jambo la kawaida bila kuwapo juhudi zozote za kuandaliwa kuwa viongozi wa baadaye.

Kwa ujumla, wakiendelea na mtindo wa kushinda kwenye mitandao ya kijamii na kuandika mambo ambayo hayana maana badala ya kutafuta fursa mbalimbali zikiwamo za uongozi, wajiandae 'kupotea'.

Sina maana kwamba mitandao ya kijamii ni mibaya, bali inategemea ni namna gani ambavyo mtu anaitumia. Kwa kiwango kikubwa vijana wamekuwa wakiitumia kutukanana na hata kuweka picha zisizofaa.

Vijana wanatakiwa kuwa sehemu ya maendeleo kwa nchi yao badala ya kubaki wakitumiwa na baadhi ya wanasiasa au wenyewe kushinda kwenye mitandao ya kijamii wakifanya vitu ambavyo havina manufaa.

Mazingira hayo ya kushinda kwenye mitandao ya kijamii bila kazi ya muhimu, inakuwa ni rahisi kutumiwa na watu mbalimbali wakiwamo wanasiasa wanaopenda kufanikisha mambo yao kupitia kwao.

Sio siri kuwa wapo wanaowashawishi vijana, ilhali hawataki kuwaruhusu wakaribie au wawanie nafasi wanazoshikilia. Hivyo ni vyema vijana ambao kimsingi ni rika lenye nguvu nyingi, watafakari na kuchukua hatua sahihi.

Unapowasikiliza wanasiasa, hawakosi kuwataja vijana. Wanawataja na kuwapa ahadi nyingi zisizotekelezeka, ili waingiwe na ari ya kutekeleza matakwa ya wanasiasa hao na kumbe mwisho wa siku wanabaki walivyo.

Baadhi ya wanasiasa wanaweza kuwahadaa na kujikuta wakiingia katika makundi ambayo wakati mwingine huhusika kwenye vurugu, mradi malengo yao yatimie, hali ambayo hujikuta matatizoni.

Ninadhani umefika wakati sasa vijana wenyewe kujiongeza na kutambua kuwa wao ni taifa la kesho, hivyo wasikubali kubweteka au kutumika vibaya, badala yake wawe tayari kuandaliwa kwa manufaa ya taifa lao.

KWA MASLAHI YA TAIFA

# Jicho la haki la Samia liangazie haki ya kuchagua, kuchaguliwa



Na Pascal Mayalla

**5.-(1) Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na minane anayo haki ya kupiga kura (na kupigiwa kura) katika uchaguzi unaofaywa Tanzania na wananchi.**

LEO ninaendelea na sehemu ya pili ya mada hii niliyoianza wiki iliyopita kuhusu wema wa Rais Samia Suluhu ambaye amejipambanua ni mpenda haki na mtenda haki.

Na jinsi anavyoliponya taifa kupitia wema wake na kutenda haki kwake, nikaahidi kuanzia wiki hii nitaangazia baadhi ya vifungu vya katiba yetu, vinavyonyima haki, vilivyochomekewa kimkakati ndani ya katiba yetu ili kuvihalalisha kikatiba, wakati kiukweli kabisa vifungu hivyo ni batili na vimechomekewa kinyume cha katiba.

Kwa kuvimulika, ni matarajio yangu kwamba jicho la haki la Mama Samia litaviona na vitaondolewa ili kuwatendea haki Watanzania.

Nimepata bahati kusomea sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na hawa ni baadhi ya walimu wetu, kina Prof. Issa Shivji, Prof. Palamagamba Kabudi, Prof. Sifuni Mchome, Dk. Ibrahim Juma (sasa Profesa na ndiye Jaji Mkuu) Prof. Safari, Prof. Gamaliel Mgongo Fimbo, Prof. Chris Peter Maina, Dk. Hamud Majamba, Dk. Tulia Akson, (sasa ni Spika wa Bunge, wakati huo hata udaktari alikuwa hajaupata) kwa kuwataja wachache.

Walitufunza moja ya maeneo magumu sana kwenye fani ya sheria, ni eneo la kutafsiri katiba na sheria, Kiingereza wanaita "Legal Interpretations" na kutokana na umuhimu wa eneo hili, kwa mujibu wa katiba yetu, taasisi pekee yenye mamlaka ya kutafsiri sheria ni Mahakama, upande wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Tulifundishwa katika kutafsiri sheria, mahakama inaangalia nia na dhamira ya mtunga katiba na mtunga sheria, au alidhamiria nini kutunga kipengele hicho kinachohitaji kutafsiriwa, hivyo ili kutafsiri kifungu chochote cha katiba, lazima kwanza wewe mfasiri uvae viatu vya mtunga katiba.

Kifungu cha Katiba ninachotaka jicho la Mama Samia likiangazie, kwanza ni Ibara ya 5 ya msingi wa haki na dhamira ya mtunga katiba.

5.-(1) Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na minane anayo haki ya kupiga kura (na kupigiwa kura) katika uchaguzi unaofaywa Tanzania na wananchi.

21.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 5, ya 39 na ya 67 ya Katiba hii na ya sheria za nchi kuhusiana na masharti ya kuchagua na kuchaguliwa, au kuteua na kuteuliwa kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria.

Kifungu hicho ndio nia na dhamira ya mtunga katiba kwamba "kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kwa hiari yao".

Kumbe haki hiyo ya kikatiba iliyotolewa na ibara 5 na Ibara ya 21 hiyo, imekuja kufanyiwa marekebisho kinyume cha katiba kwa kuipora haki hiyo ya msingi kwa kuichomekea ibara ndogo mbili ya 39 na 67 zinazoipora kabisa haki iliyotolewa na Ibara ya 5 na Ibara ya 21 ya katiba.

Ibara hizo zinasema: 39 -(1) Mtu hatastahili kuchaguliwa kushika kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kama- (c) ni mwanachama, na mgombea aliyependekezwa.

67-(1) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo- (b) ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa.

Kwa mtu wa kawaida tu ambaye sio mtaalamu wa kuisoma katiba, utakiona vipengele hivyo vya katiba viko sawa kabisa vinatoa haki kwa kila Mtanzania mwenye sifa, kuwa huru kushiriki katika siasa kwa haki ya kuchagua na kuchaguliwa, kumbe haki hizo zimeporwa kwa kuchomekewa sharti la kudhaminiwa na chama cha siasa, ambalo sio dhamira ya mtunga katiba.

Masharti haya ni kinyume cha katiba ya JMT ya mwaka 1977, ni kinyume cha Universal Declaration of Human Rights, ni kinyume cha The United Nations Human Rights Committee, ni kinyume cha African Chatter of People and Political Rights hivyo tunamwomba Rais Samia, lile jicho lake la haki, pia likiangazie kipengele hiki cha dhulma, ili kuwatendea haki Watanzania.

Katiba ni mali ya wananchi, katiba hiyo inatungwa kwa misingi ya haki, Katiba imeweka haki ya wananchi kuchagua na kuchaguliwa na ikazifungia haki hizo kwa kuweka "ring fencing" Bunge lilipata wapi mamlaka ya kuipindua katiba ya nchi?

Tukutane wiki ijayo, na kwa vile hii ni 'issue nyeti' ya kikatiba na kisheria, tutakwenda mdogo mdogo, nikiwapitisha taratibu, hatua kwa hatua ndani ya katiba yetu ilitokeaje kipengele hicho kikachomekewa ndani na katiba yetu ilhali tuna wanasheria ma nguli wa katiba

**Wasalaam**
**0754270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hakika Tuzo ya Mo Ibrahim kwa Chifu Hangaya



Na Joseph Kulangwa

**Hata alipoapa Rais Samia, akaahidi kuendeleza alipoachia Dk. Magufuli ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya kimkakati, lakini pia kuendeleza utulivu na amani kama tunu ya Taifa hili tuliyoachiwa na Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere.**

RAIS John Magufuli alipoaga dunia Machi 17 mwaka jana, nilipatwa na mshtuko na kujingwa na simanzi, nikajiuliza kwa nini ghafla hivi, ingawa kulishakuwa na minong'ono na uvumi wa hapa na pale kuhusu afya yake.

Hata hivyo, viongozi wa juu akiwamo Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, walitutia moyo Watanznaia na hata kufikia kutupa salamu za Rais, wakituhakikishia kuwa alikuwa na afya njema na anachapa mzigo kama kawaida.

Hivyo, usiku ule alipotangaza Makamu wa Rais wakati huo, Samia Suluhu Hassan, kwamba Dk. Magufuli hatunaye tena kutokana na afya yake kudorora kwa tatizo la umeme wa moyo, tulishtuka na kuamini na kujipa moyo.

Tulijipa moyo kwa kuwa tuliamini kuwa ni kwa mapenzi yake Mola, akamtwaa mja wake na ni kwa kuwa ndiye mtoaji na mtwaaji. Tukaangalia mbele na kukubali kuapishwa kwa Samia kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia.

Mimi niliamini kwamba tunaendelea na awamu ya tano aliyoiacha ghafla Dk. Magufuli, lakini ghafla nikasikia hii sasa ni awamu ya sita, awamu ya Rais Samia. Kwa kuwa mambo yalikuwa yanaendelea kwa amani na utulivu, nikaacha kuhoji, nikijua serikali ni ile ile.

Hata alipoapa Rais Samia, akaahidi kuendeleza alipoachia Dk. Magufuli ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya kimkakati, lakini pia kuendeleza utulivu na amani kama tunu ya Taifa hili tuliyoachiwa na Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere.

Ni vyema kwamba Rais Samia pamoja na kuendeleza miradi na tunu hizo, akaamua kuja na mfumo wake wa kuongoza nchi, akaifungua na kujichanganya na wapinzani na makundi mengine muhimu ya kijamii na kiuchumi, kuzungumzia na kujadili mustakabali mpana wa Taifa hili.

Vijiweni pamoja na kutambua jinsi Rais anavyotupeleka vizuri kwa amani, mshikamano na upendo mkubwa kama mama yetu kabisa, nikaendelea kuhoji na kuuliza inakuwaje hii ni awamu ya sita na si ya tano?

Nikihoji hivyo, nikitaka kujua kuwa mbona awali alipoapa Dk. Magufuli kwa mara ya pili, baada ya ushindi mwingine wa mwaka juzi, nilijua sasa awamu ya tano itamalizika 2025, iweje ya sita imeingia ghafla? Nikajipa jibu kuwa kumbe awamu ya sita itamalizika mwaka 2030.

Na itakuwa ni mara ya kwanza kwa kiongozi kumaliza awamu yake akiitumikia chini ya miaka 10 kama watangulizi wake walivyofanya kuanzia kwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi kuja huku kwa Rais Samia, kwani alianza mwaka jana, hivyo mpaka 2030 atakuwa na miaka tisa tu.

Baada ya kuukubali ukweli huo, nikajiuliza tena, hivi inakuwaje kwa wale wabunge walioteuliwa na Dk. Magufuli? Inakuwaje wanaendelea kuwa wabunge wakati aliyewateua alikuwa ni wa awamu ya tano na hii ni ya sita, ambayo ilishateua wabunge wake takriban watatu?

Yawezekana kabisa hivi sasa watu wanasema Mama kabakiza nafasi moja ya wabunge wa kuteuliwa naye, lakini mimi bado inanipa shida, kwamba inakuwaje ahesabiwe na wake asiowateua yeye, tena wa awamu nyingine?

Pengine ndiyo sababu watu wanapigia kelele Katiba Mpya, kwamba inaweza kuja na majibu ya haya nami nikaelimika kuhusu siasa zetu. Inanipa shida sana, kwamba awamu ya sita inakuwa na wabunge wa awamu ya tano.

Uzuri ni kwamba sisi Watanzania hatuna shida, mradi mambo yanavyokwenda shwari, tunakula, tunavaa, tunalala na kuamka salama na hayo ndiyo mahitaji yetu ya msingi, mengine ni kuwaachia wanasiasa wayamalize wao.

Ila ninaendelea kumshukuru Rais, kwamba anakwenda vizuri licha ya hayo mengine yanayohitaji marekebisho madogo madogo tu, hasa hili la kuanzisha kikosi kazi cha maridhiano, ni jambo mwafaka kabisa litakaloifikisha nchi pazuri.

Mama Samia kwa mwendo huu sidhani kama atakapomaliza muda wake atapishana na Tuzo ya Mo Ibrahim ambayo huangalia utawala bora katika mataifa yetu haya ya Afrika. Tumsaidie, tumwombee, ili aje na Tanzania inayoendana na mema hayo.

**Alamsiki!**

# Ijue siri kushamiri vitendo vya ukatili



FAMILIA ni msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo yanahitaji watu waadilifu. Uadilifu huo unajengwa kuanzia ngazi ya familia.

Tunaishi katika jamii ambayo kuna migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Hali kadhalika, ombwe la malezi ya watoto ni kubwa katika jamii yetu ya leo, kwani wazazi wengi hawana muda na watoto wao.

Hali hii inaathiri sana makuzi ya watoto na kuchangia ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Ukatili ni tatizo la kimaadili, hivyo, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinapoongezeka katika jamii ni kiashiria cha mmomonyoko mkubwa wa maadili.

Tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Wanasaikolojia wanasema, zaidi ya asilimia 6 ya wewe na mimi tulivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Hivyo, watu wakatili wametengenezwa katika familia. Ni vema ieleweke wazi kuwa, jukumu la kujenga jamii na taifa letu ama kulibomoa, tunalo sisi wazazi, walezi na wanajamii.

Wakati umefika sasa jitihada za kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto zisiwe za kutoa matamko, kutengeneza mabango, fulana au vipeperushi tu na kutafuta umaarufu, bali jitihada hizi lazima ziende sambamba na dhana nzima ya malezi katika ngazi ya familia. Ustawi wa taifa unaanzia nyumbani kwa kuwa uhai wa taifa unategemea uhai wa familia.

**Malezi ya mtoto**

Mtoto ni malezi. Kauli mbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu wa 2022 inasema, "Tuimarishe ulinzi wa mtoto; tokomeza ukatili dhidi yake". Mlinzi namba moja wa mtoto ni mzazi. Ni wajibu wa baba na mama kuwapa watoto malezi bora. Malezi bora ni ulinzi, ufunguo na urithi wa maisha kwa mtoto.

Taasisi, jamii na taifa bora la kesho linategemea malezi bora yanayotolewa na taifa bora la leo. Malezi bora huanzia katika ngazi ya familia.

Malezi bora ndiyo mwelekeo sahihi wa maisha ya mtoto, kwani kesho bora ya mtoto inajengwa na leo bora ya wazazi bora.

Familia ni msingi na kitengo kinachomtengeneza mtoto kiroho, kimwili na kitabia (attitudes). Vitengo vingine kama taasisi za dini au shule husaidia tu na kuendeleza msingi uliojengwa na wazazi.

Kwa hiyo, kazi ya vitengo vingine inaweza kuwa nyepesi au ngumu kutegemea na jinsi kitengo cha msingi yaani familia kilivyotunza wajibu wake wa malezi. Wazazi wanapaswa kuwa mfano bora wa matendo, kauli na mienendo yao. Watoto wa leo ni raia na viongozi wa kesho; ndiyo watakaokuwa sifa au aibu kwa wazazi wao, kwa familia yao, kwa jamaa na taifa lao.

Waswahili wanasema, "mtoto umlevyo ndivyo akuavyo". Ni wajibu wa wazazi kuwapa watoto wao malezi yatakayowaandaa kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na binadamu wengine. Wazazi msikwepe wajibu wa kukemea pale inapobidi. Watoto wote wasioadibishwa na wenye tabia mbaya ni udhia, mzigo, karaha, na fedheha kwa wazazi na jamii. Ukimdekeza mwanao iko siku atakuaibisha na kukusababishia maumivu usiyoyatarajia.

Mtoto mwenye malezi mabaya atakuwa na maisha magumu hapo mbeleni. Watu wasiowajibika, magaidi, wakatili, wanyanyasaji, vibaka, walevi, kundi la watoto linalojiita, "Watoto wa Ibilisi" na "Panya Road" kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari siku za hivi karibuni, wahuni wa kila aina tulionao leo ni matunda ya malezi mabaya.

Migogoro ya ndoa huchangia katika kutengeneza kizazi cha watu wakatili. Migogoro ya ndoa huwakosesha watoto haki ya kufurahia maisha na kuwafurahia wazazi wao.

Akili (brain) ya watoto inavurugwa kwa sababu ya kubebeshwa maumivu na matendo mabaya ya wazazi wao.

Wazazi wengine wamekuwa na tabia mbaya ya kuwashirikisha watoto tofauti zao au matatizo yao, wakisahau kwamba kwa kufanya hivyo ni sawa na kuwalisha watoto sumu inayowaua kimakuzi pole pole. Kukosekana kwa utu na vitendo vya ukatili ni matokeo ya tabia ambazo huzalishwa na ndoa zenye migogoro.

**Wazazi wawe na muda na watoto**

Wazazi msiridhike tu na kule kuwapatia watoto wenu mambo ya ulimwengu huu. Watoto wenu wanahitaji uwepo wenu wakionja hisia, mapigo ya mioyo yenu, hali ya kujali na kuthamini maendeleo ya kiroho, kimwili, kiimani, kisaikolojia na kadhalika.

Upendo na muda unaopatikana kwa ajili ya watoto wenu ni zawadi kubwa isiyoweza kuthaminishwa na chochote. Mtoto hahitaji tu baba au mama bali anahitaji baba au mama anayejali na anayepatikana nyumbani. Baba na mama wasiwe kiwanda cha kuzalisha watoto na kuwatelekeza pasipo kuwajibika katika malezi.

Kuwa baba au mama ni jukumu kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wazazi wafahamu majukumu waliyonayo kwa watoto wao ili kujenga familia na jamii bora. Maadili mema ni uhai kwa familia, jamii na taifa.

Hatuwezi kuendelea kiroho, kimwili, kiuchumi, kisiasa na kijamii pasipokuwa na maadili yanayompendeza Mungu na binadamu wenzetu.

Hivyo, ili tuwe na taifa imara la watu waadilifu na wasio wakatili, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia. Baba na mama waishi katika upendo na kuonyesha tabia ya kila mtu kumjali mwenzake ili kutokupandikiza roho ya ukatili kwa watoto wao.

**Elimu dunia na elimu ya kiroho**

Watoto waliozaliwa kama raia wa dunia hii wanapaswa kutambua kuwa uraia wao halisi uko mbinguni. Hivyo, lazima watoto waandaliwe kwa ajili ya hatima hiyo pia. Jitihada za kuwapatia watoto wetu elimu dunia ni muhimu sana ziende sambamba na kuwapatia elimu ya kiroho (kuhusu Mungu) ili watoto hawa wawe baraka sasa na hapo baadaye. Malezi bora ni uwekezaji na urithi muhimu katika maisha ya mtoto.

Tutengeneze kizazi chenye kumpenda Mungu na binadamu mwingine. Vinginevyo tutakuwa na watu ambao ni mzigo usiobebeka kwa familia yenyewe, jamii na taifa kwa ujumla. Waswahili wanasema, "mkunje samaki angali mbichi".

Ukiwa mzazi au mlezi unaalikwa uwashirikishe watoto imani yako kuhusu Mungu, upendo wako kwa jirani na tumaini la maisha mema ya baadaye.

**Uhuru wa kuamua**

Tuwape watoto wetu uhuru wa kuamua, kuchagua, kutoa mawazo kuhusu maisha yao, lakini watoto wapewe uhuru wenye mipaka. Uhuru usio na mipaka matokeo yake ni vurugu, fujo na uharibifu. Tuwasaidie watoto na vijana wetu wasiendekeze tama, starehe na anasa, kiu ya mali na utajiri pasipo uwajibikaji wa kutosha. Tuwasaidie kufahamu kuwa maisha mazuri yanatengenezwa kwa kuwa na nidhamu binafsi ya maisha, juhudi, subira na uvumilivu, na kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

**Familia ni shule**

Familia ni kitovu cha malezi, shule ya Neno la Mungu, sala na kitalu cha maadili mema. Wazazi tunapaswa kuwa mfano mwema kwa watoto wetu, kwani watoto hujifunza zaidi kwa kuona na kusikia.

Ikumbukwe kwamba, siku zote matunda mema hutoka katika mti bora. Watoto wenye malezi bora; walioelimishwa kumcha Mungu watakuwa na utii, upendo, na msaada mkubwa kwa wazazi wao katika umaskini na uzee wao na kufanyika baraka kwa watu wengine pia. Suala la malezi katika ngazi ya familia ni ajenda muhimu katika jitihada za kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

JUNI 19, 2022

Nipashe


**Baba, Mama na Mwana**

*Jumapili*



Ukurasa 14

## Makange ya firigisi




## KATUNIKA

Ukurasa 16





# UNA AHADI YA KUKUTANA?

## Mwanaume mavazi haya yatakupandisha hadhi

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | T | E | N | G | A |
| | A | | | A | |
| M | K | E | | N | |
| | A | | U | D | A |
| | S | | | I | |
| T | A | M | K | A | |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UMA, SANDA, TAMKO, KANDIA, TAMBUA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa shambani na mama yake wakipalilia mihogo. Mama yake alikuwa akilima kwa haraka, lakini Juma alikuwa akilima taratibu sana.

Mama yake alimwambia aongeze nguvu ili wamalize haraka wawahi kurudi nyumbani.

Mama: Juma jitahidi kulima kwa haraka ili tuwahi kurudi

Juma: Mama lakini mwalimu alituambia kuwa 'haraka haraka haina baraka' ndio maana nalima taratibu.

Mama: Mwanangu huo ni msemo tu unaoeleza kwamba kila kitu kinatakiwa umakini, lakini wakati mwingine inahitajika haraka ili kuwahi kazi nyingine.

SWALI

Zao la tunda linalopatikana katika mkorosho linaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kilichojificha 'kuagana na umaskini'

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu siri zilizojificha kwenye fedha. Wiki iliyopita nilikudokeza kwamba fedha kama fedha haipendi kutumiwa, bali inataka kuongezwa au kuwekezwa.

Na kwamba kwa kadri unavyopunguza matumizi na kuongeza uwekezaji, ndivyo utakavyoongeza fedha yako. Leo nikupe siri ya nne kubwa na atakayeishika ataagana kabisa na umaskini!

Kwanza, zielewe njia kuu zinazotupatia kipato ambazo ni kuajiriwa, kujiajiri mwenyewe na kufanya biashara au kuwekeza.

Kuajiriwa ni pale unapoingia mkataba na mwajiri anayekupangia kazi ya kufanya na kiasi cha malipo ya kila juma au kila mwezi. Pia unaweza kupatiwa marupurupu mengine kutegemea na mkataba wa ajira yako. Njia hii ndiyo inayotegemewa na watu wengi.

Kujiajiri mwenyewe (mjasiriamali). Ni njia ya pili inayopigiwa debe sana na viongozi wakiwahimiza vijana wanaomaliza vyuo kujiajiri wenyewe kwa sababu ya upungufu wa ajira.

Anayejiajiri mwenyewe ni yule anayeanzisha shughuli ya kiuchumi kwa mtaji mdogo au mtaji wa kati na kusimamia mwenyewe. Kundi hili linajumuisha mafundi stadi mbalimbali, wachuuzi, wakulima, wafugaji, wasafirishaji na kadhalika.

Kundi hili kipato chake kinatokana na kazi zinazofanyika. Hakuna wa kukulipa mshahara isipokuwa wewe mwenyewe. Katika kundi hili unajikuta unafanya kazi kwa bidii na kwa saa nyingi hata zaidi ya wakati ulipokuwa umeajiriwa na mtu mwingine. Tofauti hapa ni kwamba fedha yote unayopata inakuwa ya kwako!

Njia ya tatu ni wale wajulikanao kama wafanyabiashara wakubwa. Mfanyabiashara mkubwa ni yule aliyefikia kiwango ambacho huajiri watu wengine wamtumikie na kumwingizia kipato naye huwalipa mshahara. Hujiwekea mfumo ambao unaifanya biashara kujiendesha na kujiongeza na ndio sababu huishia kuwa mfanyabiashara mkubwa.

Njia ya nne ya kujiingizia kipato ambayo ni tofauti kabisa na hizo nizizotaja hapo juu, ni kuwa mwekezaji. Huyu ni mtu anayenunua hisa toka kwenye kampuni na mashirika mbalimbali, au anaanzisha shughuli ya kiuchumi ambayo anauza hisa na kujipatia mtaji mkubwa wa kuendesha shughuli zake.

Watu wengi hawafahamu njia hii ya uwekezaji, hawafahamu hisa ni nini na zinawezaje kumpatia kipato. Hii inatokana kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa elimu kuhusu uwekezaji na matumizi ya fedha kwa jumla.

Huko Ulaya na Marekani, watu wamewekeza fedha zao katika kampuni kwa kununua hisa na hatimaye kuwa wamiliki wa kampuni hizo.

Jitahidi kupata elimu kuhusu uwekezaji na hisa katika semina zinazofundisha masuala hayo ili ufanikiwe katika malengo yako kiuchumi. Tafuta vitabu na majarida ya mafunzo hayo kwa kuzingatia uwekezaji hapa nchini kwetu.

Zipo tabia na mwenendo ya fedha. Fedha huwafuata wale wanaofanya shughuli zao wenyewe kwa sababu fedha hupenda mtu anayejiamini. Ufafanuzi hapa ni kwamba kuna watu wanafanya shughuli zao wenyewe kwa sababu hawana njia nyingine ya kujikimu kimaisha na mara wapatapo ajira huenda huko. Watu wa jinsi hii siyo hao ambao fedha inawafuata.

Ninazungumzia watu walioacha ajira au kumtegemea mtu fulani na kwenda kuanzisha shughuli zao wenyewe, yaani walioamua kujitegemea.

Unapoajiriwa kipato chako kinapangwa na mwajiri wako, muda wako unadhibitiwa, na ili ufanye shughuli nyingine, aidha utoroke kazini au udanganye saa ya kufanya kazi. Na mara nyingine hapo hapo kazini ukawa unafanya mambo yako kama mwajiri wako hakusimamii kwa karibu.

Watu wengi ambao wamefanikiwa sana kiuchumi hawajaajiriwa. Ndio, kuna watu ambao wanafanya shughuli zao wenyewe na bado wana mahangaiko makubwa ya maisha.

Hata hao waliofanikiwa iliwachukua muda na uvumilivu mwingi. Hakuna mtu aliyeajiriwa na kupata mafanikio makubwa ya kiuchumi labda awe ni mdokozi!

Kuna waajiriwa ambao ni wakurugenzi wakuu wa kampuni kubwa na hulipwa fedha nyingi. Usisahau ameajiriwa na yule anayemlipa mshahara anatengeneza fedha zaidi ndio sababu anamlipa mshahara mkubwa.

Ukweli huu unaweza kuwasumbua baadhi ya watu na kujiuliza kama wote tukiamua kujitegemea itakuajе? Sijasema kuwa kuajiriwa ni jambo baya, hasa! Mkazo hapa ni kuwa huwezi kufanikiwa sana kiuchumi kama umeajiriwa kwa sababu kipato chako unapangiwa.

***Kwa leo niishie hapa. Wiki ijayo nitamalizia kwa kuelezea nini kifanyike. Una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Kubana matumizi ni sawa, tatizo lipo katika utekelezaji

BAJETI pendekezwa ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 imeshawasilishwa bungeni na sasa wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi, wanaichambua na kushauri mambo mbalimbali ambayo yatamnufaisha mwananchi.

Pamoja na mambo mengine, bajeti hiyo imejikita katika kubana matumizi ya serikali kwa kupunguza idadi ya vigogo wanaotakiwa kununuliwa magari, kukopeshwa ili wafanye matengenezo wenyewe na kununua vipuri, lakini kupunguza gharama za mafuta.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha mapendekezo hayo ya bajeti Juni 14, mwaka huu, alisema serikali ilibaini fedha nyingi inapotea kwenye kugharamia mafuta, vipuri na kila ofisa mwenye cheo cha kupewa gari kuwa na gari.

Alieleza mifano kuwa wakati mwingine wanakwenda kuhudhuria mkutano mmoja, lakini kila mmoja anasafiri kwa gari lake na dereva wakati wangeweza kutumia gari moja, jambo linaloendelea kuongeza gharama.

Alisema mabosi wengine wanasafiri kwenda mkoa fulani kwa ndege lakini gari linasafiri kwa barabara likiwa na dereva ambalo hutangulia siku moja au mbili kabla, jambo linaloendelea kuwabebesha Watanzania mzigo.

Pia, viongozi husafiri na kukusanyika kwenye mkutano kwa siku kadhaa au nusu siku, wakati wanaweza kufanya kwa kutumia mtandao kuliko kutumia gharama nyingi kwenda eneo la mkutano.

Eneo lingine aliloligusia ni ununuzi ambao umekuwa ukiigharimu serikali kwa kuwa mara nyingi haufanyiki kwa kuangalia bei za soko kwa wakati huo, bali muhusika huweka bei za juu kutokana na taratibu zenye urasimu ikiwamo kucheleweshewa malipo.

Jitihada za kubana matumizi hazijaanza kwenye bajeti hii, bali miongo mingi iliyopita. Kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, anakiri kwamba alichukua hatua kama hizo mwaka wa fedha 1989/90 kwa kubana matumizi, akiwafuta kazi watumishi zaidi ya 300 wa ATC (sasa ATCL) na kufunga ofisi zao sita nje na ndani ya nchi.

Vilevile, wakati wa awamu ya nne ya Rais Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu wa wakati huo, Mizengo Pinda, alielekeza kupunguza matumizi kwa viongozi kuacha kununua mashangingi na badala yake watumie magari ya kawaida ili kupunguza gharama.

Jambo hilo lilipata upinzani mkali kiasi cha kushindwa kutekelezwa na kuendelea kama awali kwa mashangingi ya mamilioni kununuliwa kila uchao, na kwa sasa ndiyo kuna magari ya kifahari zaidi wanayotembelea viongozi, ni ya kisasa ambayo hayana miaka mingi sokoni.

Mwananchi anaweza kujiuliza kwani wakitumia magari ya kifahari au hizo gharama zinanihusu? Kila Mtanzania anahusika kuchangia mshahara, posho na matumizi mengine ya viongozi au waajiriwa wote serikalini na mashirika ya umma.

Maumivu yapo kwa kuwa kila mmoja analipa kodi kupitia bidhaa na huduma mbalimbali, kodi ndiyo hukusanywa na kusaidia miradi ya maendeleo na uendeshaji wa serikali, lakini sehemu kubwa ya fedha ni kwenye matumizi ya mishahara na matumizi mengine.

Kwa sasa unakuja utaratibu wa kila Mtanzania mwenye miaka 18 na mwenye kipato kulipa kodi kulingana na miamala yake, na ndiyo maana umeandaliwa utaratibu wa kumiliki namba ya mlipakodi, ili iwe rahisi kulipa kokote ulipo, zote hizo zinakwenda kufanya maendeleo ya nchi.

Nia ya kiongozi anayeanzisha hilo kama alivyoeleza Waziri Mwigulu, ni njema kabsa, shida itakuwapo kwa watekelezaji ambao ndiyo wanufaika, kwamba sasa hawatafuatwa na madereva, lakini watajua uchungu wa kununua vipuri na kuweka mafuta kwenye magari.

Lazima kujifunza kwa wengine, nchi zilizoendelea viongozi wake wanagharamiwa kama wa nchi zetu hizi? Niliwahi kutembelea Bunge la Denmark, niliona baiskeli nyingi, niliuliza nikaambiwa baadhi ya mawaziri wanazitumia kwenda kazini.

Tunaweza kusema kwa mazingira ya miundombinu yao na hali ya hewa kuendesha baiskeli ni kawaida kwao, lakini kwa namna nyingine wanaona ni kawaida kabisa, nasi tunaweza kuwa na namna yetu ya kupunguza matumizi.

Ni juzi tu, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, alieleza namna halmashauri zinavyogawana fedha za matumizi ya kawaifa, huku akitoa mfano wa mgawanyo ulivyofanyika kwenye Halmashauri ya Arusha.

Alishauri fedha za matumizi ya kawaida zisiachwe wao kuamua bali matumizi halisi yaangaliwe, ili zinazobakia zikajenge miundombinu ya barabara na maji ambayo inanufaisha wengi zaidi.





Ilikuwa siku ya furaha kwa ndugu na jamaa wa familia ya Magoti, baada ya mtoto wao David Magoti kufunga ndoa na Fadhila Pungu, katika Kanisa la Mennonite Tabata jijini Dar es Salaam Mei 31, 2022 mwaka huu.









MITINDO



# UNA AHADI YA KUKUTANA?

## Mwanaume mavazi haya yatakupandisha hadhi

KATIKA maisha ya kisasa suala la kukutana na watu mbalimbali ni jambo la muhimu.

Katika kukamilisha ahadi za kukutana na watu ni lazima kuwa na mpangilio maalum wa uvaaji ili kukupatia mwonekano nadhifu.

Kutokana na umuhimu wa jambo hilo, zifuatazo ni aina ya mavazi ambayo unatakiwa kuwa nayo wakati unakwenda kukutana na watu maalumu.

**Vaa kulingana na mazingira**

Unatakiwa kuvaa kulingana na mazingira ambayo unataka kwenda kukutana na watu. Hakikisha upo maridadi na umekamilika kwa kila kitu kabla ya kuanza safari.

**Sharti la kuchomekea**

Vaa shati la kubana kiasi ambalo litakufa mwonekano mzuri pale utakapochomekea.

Hakikisha usivae mlegezo na mkanda wa suruali uwe na urefu sawa.

**Usivae shati jeupe kama mwanafunzi**

Shati nyeupe ni nzuri kama unaijulia wakati unanunua hakikisha ina urembo wa aina yoyote ile au ni ya kimtindo.

**Vaa suruali nyeusi**

Inapendeza zaidi kama utavaa suruali nyeusi kwa sababu inakubali mashati ya rangi nyingi.

**Viatu vya kupangusa**

Viatu vya kupangusa vinafaa sana kwa sababu vinaleta mwonekano maridadi na wenye hadhi ya juu.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# EPUKA KUNUKA KIKWAPA

## Tengeneza 'Deodoranti' kutumia vitu



UREMBO hauhitaji gharama kubwa kama watu wengi wanavyodhani kuwa ni lazima kununua vipodozi vya gharama kubwa.

Leo tunaelekezana namna ya kutengeneza manukato ya kwapani maarufu kama deodoranti kwa kutumia viungo vya nyumbani.

Kwa watu wengi, utaratibu wa kila siku wa urembo na mapambo huanza na kuondoa harufu kwenye mwili.

Ikiwa unachagua aina ya deodoranti utakayoweka kwenye ngozi yako, kuna uwezekano utahitaji kuweka 'parabens' na kemikali zingine ambazo zinaweza kukudhuru.

Moja ya sehemu unayoweza kudhurika ni mfumo wako wa tezi kutoka kwapani, ambapo sumu inaweza kufyonzwa kwa urahisi.

Mbali na sumu na parabens, deodorants nyingi za kibiashara zina alumini, kemikali ambayo huziba mifereji ya jasho na hivyo kuzuia kutoka kwa jasho.

Kuhusu deodoranti asilia, hazina kemikali kama vile alumini na kwa hivyo hutegemea viungo vingine kuchukua unyevu na kuondoa harufu mbaya ya mwili.

**Mahitaji**

Vijiko viwili vya siagi ya shea, vijiko vitatu vya mafuta ya nazi na vijiko vitatu vya soda ya kuoka.

Jinsi ya kuandaa

Unayeyusha baadhi ya siagi ya shea katika umwagaji wa maji, pamoja na mafuta ya nazi, kisha kuongeza soda ya kuoka na kuchochea viungo vizuri.

Weka mchanganyiko huo kwenye jokofu, kisha uweke kwenye chupa ya deodoranti na uongeze mafuta muhimu kulingana na harufu unayopenda. Unaweza kuweka moja wapo kati ya haya.

Mafuta ya lavenda ni antifungal inayojulikana kutibu magonjwa. Mafuta ya mti wa chai huzaa harufu nzuri ambayo ni ya kupambana na bakteria na mafuta ya limao.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Makange ya firigisi

MAPISHI ya firigisi ni rahisi kupika na ni chakula cha haraka ambacho kinaweza kuliwa wakati wowote.

Mahitaji

Firigisi nusu kilo, karoti iliyokwanguliwa moja,nyanya nusu kopo, kitunguu maji kimoja kikubwa,

tangawizi na kijiko kimoja cha chai.

Pilipili hoho moja iliyokatwa katwa, limao nusu kipande, chumvi curry powder nusu kijiko cha chai, unga wa chili robo kijiko cha chai na mafuta.

Matayarisho

Safisha firigisi kisha zikate vipande vidogo vidogo.

Zichemshe pamoja na chumvi, limao na nusu ya tangawizi na swaumu mpaka ziive, hakikisha unabakiza supu kidogo.

Baada ya hapo kaanga vitunguu mpaka viwe vya brown kisha tia tangawizi na swaumu iliyobakia na kaanga kidogo kisha tia nyanya.

Zipike mpaka ziive kisha tia spice zote pamoja na chilli. Zipike kidogo kisha tia firigisi (bila supu kwanza) zichanganye vizuri na uzipike kidogo.

Baada ya hapo tia carrot na hoho na supu iliyobakia. Vipike pamoja mpaka viive na supu ibakie kidogo sana. Malizia kwa kutia coriander na uipue na hapo firigisi zako zitakuwa tayari kwa kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu yako

KILA mawio tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani, ambayo kwa namna moja ama nyingine yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyonayo katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana siyo yale yatakayofanyika kesho wala keshokutwa, kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Na leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni miongoni mwa vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hasa pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yapo baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili, mtaalamu huyo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake.


Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vyema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.



## Jinsi ya kutumia birika la chai la kioo




MAISHA ya kisasa yanakwenda sambamba na wepesi wa kufanya jambo kwa muda mfupi.

Birika la chai la kioo ni chombo kilichotengenezwa kwa ajili ya kumrahisishia mtu kuchemsha chai kwa haraka zaidi kuliko kutumia aina nyingine ya chombo. Kutokana na umuhimu wake, hizi ni baadhi ya njia za kutumia birika la kioo kwa ajili ya kufanya lidumu kwa muda mrefu.

1: Usiweke karibu na jiko la gesi, moto au kwenye oveni.


2: Usiwashe kama birika halina maji kwa sababu inaweza kuharibu vifaa vya ndani vinavyoruhusu joto.

Ili kulinda dhidi ya moto, mshtuko wa umeme, au jeraha, usitumbukize waya ya umeme, plagi za umeme au kifaa cha kuwekea kwenye maji au vimiminika vingine.

3: Daima jihadhari kumimina taratibu maji yanayochemka, weka kwa uangalifu bila kubonyeza kitufe cha mfuniko.

4: Ukimaliza hifadhi birika katika eneo kavu na salama.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
MJINI KELELE ZA 'MALIMBUKENI' WA UBINGWA ZIMEZIDI BORA KIJIJINI
NASKIA HUKO BUSHI KILA NYUMBA WAMEFUNGUA TAWI LAO!
SH'KAMOO!'
!
JIMBO
NAJIANDAA KUHESABIWA WE PITA TU
DEREVA JALI MUDA BHANA!
NYIE WOTE MNAMSHAMBULIA KONDA WANGU NIKAE KIMYA
MSHACHUKUA MARA NNE, WAMETESEKA MIAKA MINNE, LEO WAMELIFUMANIA MIPOVU INAWATOKA!
WEWE TAZAMA MBELE MAMBO YA USHABIKI HAYAKUHUSU
NASKIA WANAULIZIA BEI YA BAKULI SIJUI NDIO TAYARI?
KWANZA KOMBE NASKIA 'YUZIDI' TOKA TANDALE
MSHUKURU SHOGA'AKO MINYUNO UJAPOKEA SIMU KANIFUNGIA KWAKE
SEMA ULIKOLALA STAKI POROJO ZAKO 'BABA KEI'
KAJUA NIKIJA UTATOKEA 'MSIBA'
WATU TUMEONA 'MANYWELE' SEMBUSE 'MAYELE' KUTWA YEYE TU!
SOKONI
EMBU TETEMA KAMA MAYELE TUMFUKUZE "JINI GERE"
NANI ANAONA GERE? UNANTAFUTA LA ROHONI, WE HANGAIKA TU!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...HERI YA UKWELI UNAOUMIZA, KULIKO UONGO UNAOFARIJI...

# Wahamiaji Uingereza kuwekewa vifaa vya kielektroniki

**LONDON,** UINGEREZA

BAADHI ya wahamiaji wanaoomba hifadhi nchini Uingereza, waliofika kwa kutumia boti au nyuma ya lori wanaweza kutambulishwa kielektroniki.

Kulingana na Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani, ilisema jaribio hilo jipya litakalodumu miezi 12, linaweza kuathiri watu wazima.

Watu wa kwanza kutambulishwa wanaweza kuwa watu waliofanikiwa kupinga kupelekwa Rwanda baada ya kuwekewa pingamizi katika mahakama ya Ulaya.

Mpango wa kuwekewa vifaa vya kielektroniki unakuja siku chache baada ya safari ya kwanza ya ndege iliyokuwa ikichukua waomba hifadhi kutoka Uingereza hadi Rwanda kusitishwa.

Ofisi ya Mambo ya Ndani ilisema jaribio hilo lililoanza siku ya Alhamisi nchini Uingereza na Wales, litasaidia mawasiliano ya mara kwa mara na waomba hifadhi.

Watu ambao wametambulishwa wanaweza kuwa chini ya amri ya kutotoka nje, na wale ambao watashindwa kutii masharti yao wanaweza kurudishwa kizuizini, au kufunguliwa mashtaka.

Mwongozo huo ulisema wale ambao wamearifiwa kwamba wataondolewa Uingereza wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kutoroka.

# Ulaya kushuhudia joto kali

**PARIS,** UFARANSA

NCHI za Ufaransa, Uhispania, Ujerumani na mataifa mengine ya magharibi mwa Ulaya jana zilishuhudia joto kali katika mwezi huu wa Juni.

Joto hilo lililoanza mwisho wa juma linatarajiwa kuvunja rekodi kwa kuwa kali zaidi.

Hali hiyo imezusha wasiwasi wa kutokea moto kwenye misitu na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Nchini Ujerumani, viwango vya joto vitafikia nyuzi joto 30 za kipimo cha Celsius.

Hali ya joto kali tayari imeanza kushuhudiwa katika maeneo kadhaa ya Ufaransa ambako juzi kulikuwa na zaidi ya nyuzi joto 40 za kipimo cha Celsius.

Maofisa wa zimamoto nchini humo wanaendelea kukabiliana na moto unaoteketeza misitu.

Nchini Uhispania, moto uliunguza takribani hekta 9,000 za misitu katika mkoa wa Sierra de la Culebra.

**DW**

# Uingereza yakiri Russia inasonga mbele

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI mkuu wa Uingereza Boris Johnson, amesema majeshi ya Russia yanazidi kusonga mbele na kunahitajika msaada kuwaondoa katika uchovu.

Akizungumza baada ya juzi kufanya ziara ya kushtukiza mjini Kyiv, alisema nchi yake itaendelea kuonyesha kuunga mkono Ukraine.

Alionya hatari iliyopo kutokana na hali ya uchovu inayotanda duniani kote kutokana na vita inayoendelea nchini Ukraine.

"Warussia wanazidi kusonga mbele inchi kwa inchi na ni muhimu kwetu kuonyesha kile tunachojua kuwa kweli ambacho ni kwamba Ukraine inaweza kushinda na itashinda," Johnson aliwaambia wanahabari.

Aliongeza "Wakati uchovu wa Ukraine unapoanza, ni muhimu sana kuonyesha kuwa tuko nao kwa muda mrefu na tunawapa ujasiri wa kimkakati wanaohitaji,"

Alisema itakuwa janga ikiwa Rais wa Russia Vladimir Putin angeweza kupata miji iliyo kusini mwa Ukraine na Donbas.

Waziri mkuu huyo pia alisema anataka kuweka wazi Uingereza inaunga mkono Waukraine katika azma yao ya kuwafukuza Warussia.

**RUSSIA INALENGA KUSONGA MBELE ZAIDI**

Taarifa kutoka Wizara ya Ulinzi ya Uingereza, inadai kuna dalili Russia imeanzisha upya juhudi zake za kusonga mbele kusini mwa mji wa mashariki wa Izyum katika saa 48 zilizopita.

Ilisema taarifa hiyo kuwa lengo lake ni kupenya ndani zaidi katika eneo la Donetsk na kuzunguka mji uliozingirwa wa Severodonetsk kutoka kaskazini.

Iliongeza kuwa raia wa Ukraine walionaswa katika mji huo wana uwezekano wa kuwa na mashaka ya kutumia njia za kibinadamu ambazo zimependekezwa na watu wanaotaka kujitenga na maofisa wa Russia.

Iwapo raia wa Ukraine walionaswa hawatakubali ofa ya kuondoka kupitia ukanda huo, Russia ina uwezekano wa kudai uhalali wa kutotofautisha kati yao na shabaha zozote za kijeshi za Kiukreni katika eneo hilo.

**BBC**



Mwanajeshi wa Ukraine akiangalia daraja lilobomolewa na makombora ya Russia katika kijiji cha Ruska Lozova karibu na mji wa Kharkiv jana. **PICHA: EPA-EFE**

# Mwanaume achoma kaburi la mama mkwe

**KARACHI,** PAKISTAN

MWANAUME mmoja raia wa Pakistani, ameripotiwa kuchoma moto kaburi la mama mkwe wake aliyefariki miaka 25 iliyopita huko Layyah, jimbo la Punjab nchini humo.

Kulingana na taarifa, mwanamume huyo ambaye hakutajwa jina alimwaga petroli kwenye kaburi na kuchoma moto Mei 13, na kutishia kutuma picha za eneo hilo kwa mke wake wa zamani.

Suala hilo lilikuja baada ya mke wake wa zamani, ambaye alitalakiana naye miaka 10 iliyopita, kujitolea kuolewa tena, jambo ambalo lilimkera.

Shemeji yake ambaye alifungua kesi baada ya tukio hilo, alisema mwanamume huyo alitishia kuchoma kaburi la mamake baada ya kukasirishwa na kukataliwa na dada yake.

Msemaji wa polisi alisema kaburi hilo limepatikana likiwa na dalili za kuchomwa moto, na mtu huyo alikamatwa na atafikishwa mahakamani.

Katika ujumbe wake aliotishia kuchoma moto kaburi la mama mkwe wake, polisi walisema baada ya kupata taarifa hizo walikwenda eneo la tukio na kuwahoji wanafamilia wa binti huyo na majirani.

Kisha wakafanya kazi ya kumtafuta na kumkamata mhusika.

Polisi walisema kuwa kesi hiyo inachunguzwa na mwanamume huyo amekamatwa baada ya msako uliodumu kwa saa 24 na atafikishwa mahakamani.

Alipotafutwa na BBC, kaka ya mwanamke alisema kuwa shemeji yake alikuwa amejitolea kumuoa tena dada yake, lakini baada ya kukataliwa mara kadhaa, alikasirika na kuchoma kaburi la mama yake.

"Baada ya muda nilipata ujumbe kwenye mtandao wa WhatsApp kutoka kwenye simu ya dada yangu ikiwa na picha za kaburi la mama likiwashwa kwa gesi."

alisema alienda kaburini na familia yake na kuuzima moto huo na kutoa taarifa kwa polisi. Familia ilisema haikutaka kuzungumzia suala hilo kwa wakati huu.

"Mumuadhibu tu mshtakiwa, tunaomba hilo" walisema ndugu wa marehemu baada ya kukamatwa kwa mtu huyo.

Polisi wa Punjab walitangaza kukamatwa kwake kupitia mtandao wa Twitter na kuibua hasira kwa wananchi wengi.

**BBC**

MAKALA

# ULINZI WA WATOTO NI JUKUMU LETU KAMA JAMII NA NCHI



Na Magabilo Masambu - 0689157789

KILA ifikapo Juni 16 ya kila mwaka Afrika tumekuwa tukiazimisha Siku ya Mtoto wa Afrika. Hii ni kutokana na mauaji ya watoto yaliyofanyika Juni 16 mwaka 1976 huko Afrika ya Kusini Mtaa wa Soweto, wengi wakiwa vijana wa shule walioandamana kupinga ubaguzi wa rangi katika kupewa elimu.

Itakumbukwa kwamba Afrika Kusini ni kati ya nchi zilizoathiriwa sana na ubaguzi wa rangi kati ya wageni (makaburu) na wenyeji hasa kabila la Wazulu, ambao baada ya makaburu hao kuikalia nchi hiyo kwa muda mrefu na kuchukua mamlaka ya kiuongozi, waliendesha harakati za kuwabagua wenyeji katika huduma za msingi kama elimu na nafasi za madaraka.

Makaburu walipata elimu bora yenye manufaa zaidi kuliko elimu waliyopatiwa watoto wa kiafrika, kukawa na lugha zaidi ya moja zilizotumika kufundishia, makaburu walijifunza kwa lugha ya Kiingereza wakati watoto wa kiafrika wakipata elimu yao kwa lugha ya Kiafrikana pamoja na Kizulu.

Wakati makaburu wakifundisha watoto wao kuwa wanasheria, viongozi, madaktari, mameneja na kadhalika, watoto wa Kiafrika walifundishwa kuwa wasusi, wavuvi, vibarua na kazi nyinginezo ambazo zingeliwafanya wasipate kazi za maana katika nchi yao.

Kutokana na masaibu hayo, vijana hao mwaka wa 1976 wakaamua kuandamana katika mji wa Soweto kupinga ubaguzi wa namna hiyo, ndipo walipouawa mamia kwa makumi. Mauwaji hayo yaliibua hisia kali ulimwenguni kote na kuongeza harakati za ukombozi barani Afrika.

Wakati hayo yakifanyika, Nelson Mandela alikuwa amefungwa jela toka mwaka 1962 akitumikia kifungo gerezani alikotoka mwaka 1990 na mwaka 1994 akawa Rais wa kwanza mweusi katika nchi hiyo.

Tunapoadhimisha siku hii, tusifanyike sherehe pekee za kufurahisha genge au vijiwe lakini kama waafrika lazima tuwe na tafakuri juu ya matendo ya ovyo tunayowatendelea watoto wetu. Ukatili wa kijinsia, ubakaji na ulawiti na matendo mengine machafu juu wa watoto wetu.

Tukiendelea kuazimisha na kutoa historia nzuri juu ya siku yenyewe bila kukomesha vitendo hivyo, basi hatutakuwa na sababu ya kuendelea kuiazimisha siku yenyewe.

Siku za hivi karibuni pamoja na kwamba inawezekana vyombo vya habari vinafanya kazi nzuri sana ya kufichua maovu, visa vya ubakaji na ulawiti vimeonekana kuongezeka kwa kasi zaidi, kama nchi na jamii kwa ujumla tusipochukuwa hatua za makusudi kwa kutoa adhabu kali zaidi ikiwamo hata kifo kwa wale watakaobainika kutenda uchafu huo, basi tujihesabu hatutakuwa na taifa lenye watu wenye afya bora na maadili.

Hebu jaribu kufikiria kama mtoto wa miezi minane analawitiwa na akaharibiwa kabisa, unalea mtoto wako kwa upendo mkubwa, anaanza shule anafika kidato cha pili halafu unakuja kugundua kuna jirani yako ana miaka 50 anamlawiti mtoto wako uliyemlea na unategemea kesho na keshokutwa utakapokuwa mzee, huna nguvu akusaidie, ameshaharibiwa hafai, ni maumivu kiasi gani utayasikia moyoni?

Kibaya zaidi, matendo haya ya kishenzi hayafanywi na watu wa mbali, ukisikia kesi nyingi utakuta ni watu wa karibu, mjomba, baba mkubwa au mdogo, mwalimu, rafiki wa baba na kadhalika. Wale tunaowaamini ndiyo wanaotuharibia watoto wetu badala ya kuwalinda wanakuwa waharibifu wa kwanza.

Kuna wakati fulani mauaji ya ndugu zetu wenye ualbino yalipozidi, Waziri Mkuu wa wakati huo, Mizengo Pinda alitoa kauli ambayo iliandamwa sana na watetezi wa haki za binadamu, lakini jaribu kufikiria kama mtu anaweza kumtoa mkono binadamu mwezake akiwa hai au mtu anamlawiti mtoto na kuharibu maisha yake yote na mtu huyu ni mwenye akili timamu akionyeshwa chungwa hawezi kuita kitunguu, jaribu kufikiria kama aliyetendewa unyama huo ni mtoto wako unayempenda.

Ni kweli kwamba nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria, jambo jema kabisa, lakini sheria zinatengenezwa na kurekebishwa kila siku, tunashindwa nini kutegeneza sheria kali zaidi za kuwaadhibu wanaopatikana na hatia kama hizo?

Kama tuna uwezo wa kurekebisha sheria mbalimbali kama ambavyo juzi tulikuwa na marekebisho ya Muswada wa Sheria Mbalimbali Na. 7 ya Mwaka 2021, tunashindwaje kurekebisha sheria juu ya makosa ya namna hii ambayo yanaliangamiza taifa?

Tufanye marekebisho ili waadhibiwe kwa mujibu wa sheria kali, vinginevyo tunaliingiza taifa hili kwenye Sodoma na Gomora na Mungu aliyetupatia nchi hii nzuri atachukia, matokeo yake nchi hii itaingia kwenye laana kubwa, hatutapanda wala kuvuna, kufuga wala kuvua.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, wakati uchafu huu unaonekana kuongezeka, ndiyo wakati tunaoshuhudia pia nyumba za ibada zikiongezeka na tunategemea ongezeko la nyumba za ibada liendane na ongezeko la maadili mema katika jamii lakini inakuwa kinyume chake, inawezekana tunakwenda makanisani na misikitini kutimiza wajibu na kwamba tutazamwe na wao kama walivyo mafarisayo, inawezekana nyumba za ibada zinatumika kama mwamvuli wa kuficha matendo yetu machafu, tunasali sana ili tuonekane wema machoni pa watu huku mioyo yetu ikiwa imejaa unyama na ukatili wa kutisha.

Ushauri wangu, kwa sababu matendo haya yanatendwa na watu wetu wa karibu, basi usimwamini yeyote aingiaye nyumbani mwako hasa jinsia ya kiume maana ndiyo tunaotuhumiwa zaidi.

Marufuku baba mdogo au mkubwa, mjomba, kaka, babu au kijana wa kazi kulala na mtoto wako, awe wa kiume au wa kike. Zipo tuhuma zinazowahusu baadhi ya baba wazazi au baba wa kambo kuwafanyia ukatili watoto wao au wa kufikia, tumekuwa kama nguruwe anayezaa watoto na kuwala tena, ni jambo la kusikitisha sana. Tuwalinde watoto wetu ili waweze kutimiza ndoto zao na watakaotusaidia tukizeeka kwani watoto ni hazina kwetu.

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Msondo, Sikinde, Bima, OSS zilivyochukuliana wanamuziki



Na Adam Fungamwango

MIAKA ya 1970 mpaka mwishoni mwa miaka ya 1980 ilikuwa ni kama kilele cha muziki wa dansi Tanzania, maana ulikuwa juu sana kiasi cha kuogopwa hata na bendi za nchini Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) na hata nchini Kenya.

Wanamuziki wa Congo DR, na Wakenya waliwaheshimu mno wanamuziki wa Tanzania. Walikuwa wako juu mno kimuziki kwenye miongo hiyo miwili.

Ni baada ya kutoka kwenye miaka ambayo wanamuziki wa Tanzania walikuwa wakiiga muziki, yaani mirindimo, huku wakitunga mashairi yanayofanana na yale yanayoimbwa kwenye lugha ya Kilingala.

Ilifika wakati serikali ya Tanzania ikashtuka na kupiga marufuku bendi zote za Tanzania kuiga nyimbo au kuzibadilisha kwa namna yoyote ile na badala yake kutunga na kuimba zao wenyewe.

Hiyo ilikuwa ni miaka ya 1960. Ilipofikia miaka ya 1970, sasa ndipo hali ilipobadilika, wanamuziki wa Tanzania walianza kutunga na kuimba nyimbo zao ambazo hazikuigwa kutoka popote pale.

Ni hapo ndipo muziki wa Tanzania ulipopanda thamani, na wanamuziki kuwa na thamani na gharama kubwa.

Na ndipo lilipoanza wimbi la kuchukulia wanamuziki. Wimbi hili lilikuwa likiwazunisha wengine na kuwafurahisha wengine kama ambavyo vilivyo vipindi vya usajili kwenye mchezo wa soka.

Mchezaji anaweka kutoka Simba kwenda Yanga, wanachama na mashabiki wanakuwa wanatambiana mitaani kuwa wamemchukua mchezaji wao, huku wengine wakihuzunika na kusononeka.

Kwa wale wanasoka wanakumbuka kipindi mchezaji Ramadhani Wasso wa Simba walipodai anakwenda Ubelgiji, lakini akaibukia Yanga.

Kelvin Yondani naye alivyotoka Simba kwenda Yanga, pia Haruna Niyonzima alipotoka Yanga kuelekea Simba, vile vile Bernard Morrison alipotoka Yanga kwenda Simba.

Kuna waliofurahi na walioumia. Na hivyo ndivyo ilikuwa kwenye muziki wa dansi enzi hizo.

Wimbi la kuhama wanamuziki na kuanza kutikisa mashabiki lilianza mwaka 1977, wakati mwanamuziki mpiga gitaa la solo, Abel Bathazar alipotoka Juwata Jazz band 'Msondo Ngoma' na kuunda bendi ya Dar International.

Ilikuwa bado kidogo Muhidini Gurumo wa Msongo naye aende kujiunga na bendi hiyo, ikashindikana.

Na si wengi wanaofahamu kuwa hata Hamisi Juma 'Maalim Kinyasi' alijiunga na bendi hiyo kutoka Biashara Jazz, lakini baada ya muda mfupi, akarejea alikotoka kabla haijarekodi.

Mwaka 1978, wimbi la kuhama wanamuziki liibuka tena, baada ya robo tatu ya wanamuziki wa Dar International kwenda kuunda bendi ya Mlimani Park Orchestra 'Sikinde Ngoma ya Ukae.'

Safari hii wanamuziki wa Sikinde hawakutaka kufanya makosa, wakawachukua Gurumo na Maalim Kinyasi baada ya kushindikana awali kuwa nao walikotoka.

Mwaka 1979, Hassan Rehani Bitchuka na Selemani Mwanyiro, walitikisa nchi, walipoondoka Msondo kwenda kuungana na kina Gurumo Sikinde.

Msondo ikaenda kumchukua mwanamuziki asiye na jina wakati huo, Shaaban Dede, ambaye kwa muda mfupi tu alileta mabadiliko makubwa kwenye bendi mwaka 1980, lakini Sikinde ikapeleka pigo lingine kwa kumchukua Dede mwaka 1981. Msondo ikaenda Polisi Jazz na kumtwaa Moshi William, baadaye Tanzania Stars ikamchukua Suleiman Mbwembwe.

Ikaenda tena Dar International na kuwachukua Tino Msinge na Fresh Jumbe kuziba nafasi.

Mwaka 1984, Sikinde ambayo ilikuwa inaionea Msondo nayo ilipata mbabe wake, Bima Lee ambayo ilichukua wanamuziki tegemeo kina Dede, Joseph Mulenga, Abdallah Gama na Mwanyiro.

Bitchuka naye alikuwa kwenye safari hiyo, lakini kwa sababu zisizojulikana akasita kwenda Bima Lee.

Pigo lingine liliipata Sikinde mwaka moja uliofuata 1985, Orchestra Safari Sound walipowachukua Bitchuka, Gurumo na wanamuziki wengine waliokuja kuziba mapengo ya kina Mulenga, ambao ni Kassim Rashid, Ally Makunguru na Charles John Ngosha, wakaenda OSS na kuasisi mtindo wa Ndekule.

Sikinde nayo inaenda kwa mnyonge wake Msondo na kumchukua Fresh Jumbe kuziba nafasi, kabla ya Msondo kumpata mwimbaji Nico Zengelaka kutoka Kenya, aliyekuwa na bendi la Les Cuban.

Ndekule ilirudi Sikinde na kuwachukua Cosmas Chidumule, Max Bushoke na wengine mwishoni mwa miaka ya 1980, na hii ni baadaye Bitchuka kurejea Sikinde.

Mwisho wa siku, Gurumo na Bitchuka walirejea Msondo mwaka 1990.

Hizi ndiyo bendi kubwa ambazo zilikuwa zinachukuliana sana wanamuziki. Na mara nyingi wanamuziki hurubuniwa na kuchukua kipindi ambacho bendi huwa hazipigi kutokana na mfungo wa Ramadhani, na huanza kuonekana kwenye bendi zao mpya sikukuu ya Eid El Fitri.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

MOJA kati ya watu aliofuatana nao walionekana ni mke na mume waliokuwa wakigombana. Kwa sababu hakuwahi kuishi kwenye familia aliona ni kitu cha ajabu.

Mke alikuwa amebeba mtoto na baba anatembea huku akiongea maneno ambayo yalionekana kabisa alikuwa anataka amuachishe mtoto kunyonya. Lakini mama alikuwa hataki.

"Yaani mtoto mwaka mmoja na nusu baba Beka tumuachishe kweli?" Alilalamika mke.

"Ndiyo nimeshasema hivyo."

"Aka mwenzangu, mtoto bado huyu, kliniki wamesema mtoto anyonye maziwa ya mama hadi miaka miwili."

"Hakuna, kwani umeolewa na kliniki au mimi?" Mume alizidi kukoroma.

"Kule kuna madaktari na manesi, ni watu wa afya wanajua kila kitu." Mke alitetea.

"Sasa endelea kuwasikiliza, watakuponza."

"Eee eee bwana, usinitishe, kama unataka kwenda kwa huyo Asha wako nenda."

Mwanaume alitaka kuongea kitu, lakini akapatwa na kigugumizi.

Prince alikuwa nyuma yao, hivyo aliwaona wote wawili vizuri. Mwanaume kwa hasira alitaka kumpiga mkewe ambaye alikuwa na mtoto.

Kabla mkono haujatua mwilini, ghafla Prince aliruka kwa hatua ndefu na kuukamata, kabla haujafika kwenye shavu.

"Hallo, wewe ni mwanaume, unagombana vipi na mkeo njiani kama hivi?" Kwa jinsi alivyoushika mkono huo, baba yule hakutamka kitu chochote. Wala hakutaka ugomvi na yeye. Ni kwamba alikutana na mkono wa binadamu mithili ya chuma. Aliona kabisa huyu mwamba ni mtu wa mazoezi.

"Mama, huyu kama akikufanyia fujo tena njiani au nyumbani, au akataka kukulipizia kisasi changu kwa kukusaidia, basi kesho njoo pale kwenye duka lile lenye picha ya Bruce Lee."




**"Siyo kukupiga, hata akiendelea na mpango wake wa kutaka kumuachisha mtoto kunyonya, we njoo, halafu ndiyo atanijua mimi nani." Wakati Prince akiongea na mama yule mumewe alikuwa kimya. Alishaingiwa na woga kuwa amekutana na mtu mkakamavu na si wa kawaida.**

"Sawa baba, maana mume wangu siku hizi simuelewi, ananipiga mara kwa mara, kisa nimuachishe mtoto kunyonya, hajafika miaka miwili huyu, mimi akinipiga nitakuja kwako mdogo wangu."

"Siyo kukupiga, hata akiendelea na mpango wake wa kutaka kumuachisha mtoto kunyonya, we njoo, halafu ndiyo atanijua mimi nani."

Wakati Prince akiongea na mama yule mumewe alikuwa kimya. Alishaingiwa na woga kuwa amekutana na mtu mkakamavu na si wa kawaida. Alijua anaongopa, hafanyi kazi pale alipomwambia, ila aligundua kuwa jamaa alishamhofia, hivyo kwa kitendo cha kumwambia tu mkewe akikukorofisha aje sehemu ile, alijua hatorudia tena kumpiga na kumnyanyasa.

"Haya nendeni. We bwana, nikiona mkeo kaja kesho au siku yoyote pale dukani kwangu kuniambia kuwa umempiga au kumtukana, ndiyo utanijua mimi nani."

"Hapana mdogo wangu, nisamehe, pombe tu hizi." Akajitetea.

"Haya mshike mkeo, nenda naye nyumbani."

Akaanza kujishangaa, huruma hii ameipata wapi? Alizaliwa na kulelewa kwenye mazingira ya upweke, akiwa peke yake, na kujazwa maneno na falsafa nyingi za ushujaa, ubabe na ukatili na baba yake mzee Pokwa.

Labda yule mwanamke alivyokuwa anafanywa na mumewe alivuta picha kama ya mama yake mzazi ambaye hivi karibuni aliambiwa na baba yake kuwa aliuawa.

Hadithi ya mama yake, ilimuweka kwenye pande mbili, kuna wakati anakuwa katili, hasa kwa wote wanaohusika kumuua, lakini alianza kuwa na huruma, hasa anapoona mwanamke ananyanyasika, akivuta taswira ya marehemu mama yake.

Ghafla ndipo alipokumbuka kuwa ana kibarua kizito. Kibarua cha kwenda kutoa uhai wa mtu mmoja anaitwa Hussein. Ni moja kati ya watu ambao walihusika kumuua mama yake. Akaanza kupiga hatua za haraka haraka ili asije kuchelewa windo lake.

Akafika alipoambiwa. Ni kweli alikuwa amechelewa. Alilikuta gari ambalo aliambiwa kuwa ni la Hussein. Awali alichotaka ni kufika mapema, gari lifike wakati yeye yupo pale, alitazame windo lake vizuri. Aingie na kutoka.

"Hata hivyo hapajaharibika neno." Alijisemea mwenyewe. Alishaambiwa wajihi wake. Na pia gari alolikuta ni lile lile lililo nje ya hoteli.

Alichokuwa na uhakika nacho ni kwamba, yoyote atakayetoka hotelini hapo, mwenye umri kati ya miaka 60 hadi 65 na kuelekea kufungua mlango wa gari lile, basi atakuwa ndiyo Hussein. Picha yake pia ilikuwa mfukoni mwake, ingawa kwa wakati ule wa usiku aliona haitomfaa.

Ni dakika 15 tu zilizofuata macho yake yalimuona mtu mmoja aliyekuwa amevaa kanzu, mkononi akiwa na mkoba.

Wala hakutaka kujiuliza mara mbili kuwa alikuwa ni mzee Hussein. Alilielekea gari ambalo lilikuwa pale. Alipofika kwenye mlango ni kama alizubaa kidogo, aliangalia alikotoka na kuchelewa kufungua mlango wa gari kwa ufunguo aliokuwa nao.

Prince alikiona vizuri kichogo cha mzee Hussein vizuri mno pale alipokuwa akiangalia mlangoni. Ni kweli alikuwa akimuangalia kijana mmoja ambaye alikuwa anatoka na kusimama mlangoni, nadhani kwa sababu za kiusalama zaidi.

Ni hapo hapo alipokuwa anapahitaji. Hakuwa na muda mwingine tena. Ni risasi moja tu iliyokwenda kupenya kwenye kichogo cha mzee Hussein na kutokea mbele kwenye paji la uso. Ilimrusha pia hatua kadhaa mbele na mkoba wake.

Kwa sababu hakuwa na shida ya mkoba, Prince alichofanya ni kugeuka tu na kuondoka, huku yule kijana aliyekuwa mlangoni akitoa bastola yake na kuanza kupiga hovyo akidhani kuwa ni majambazi wamevamia kwa lengo la kumpora pesa zake. Hakuona mtu yoyote akijitokeza kuja kuokota mkoba ule, lakini hakujiamini akaendela kumimina risasi zilizowafanya watu wengi waliokuwa eneo jirani kutimua mbio.

Kilichoendelea hapo ni kwamba askari polisi baada ya kufika waliambiwa kuwa majambazi walivamia kwa lengo la kutaka kumpora pesa mzee Hussein. Walichofanikiwa ni kutoa uhai wake, lakini kijana yule alipambana sana na majambazi ambao walikuwa wengi, lakini kijana yule alipambana nao sana na kushindwa kuchukua pesa.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# Gigy Money afanya kufuru ya fedha

MSANII wa Bongo Fleva na filamu, Gigy Money, wiki hii ameangusha pati ya nguvu katika kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Gigy Money katika sherehe hiyo aliwakumbusha wasanii wenzake wa kike kujiamini kwa kila kitu kwani yeye amefanikiwa katika maisha yake kutokana na udhubutu na kuamini anachokifanya.

Baadhi ya mastaa waliohudhuria katika pati hiyo iliyofanyika Mikocheni jijini Dar es Salaam ni Hamisa Mobetto na Mimi Mars.

# KIDUME

## ANAYEMTAKA SARAFINA AJIPANGE

MSANII anayefanya vizuri katika muziki wa Bongo Fleva, Sarafina, amesema hataki kumsikia mwanaume mwenye tabia ya kumrudisha nyuma na kumpatia msongo wa mawazo.

Akizungumzia aina ya wanaume ambao wanaweza mmoja wao kuwa ni mume wake, amesema anatamani kuwa na mtu mwenye huruma, anayemuunga mkono katika kazi yake na anayejali.

"Japokuwa sipendi kuzungumzia uhusiano wangu wa kimapenzi, lakini napenda mwanaume anayeniunga mkono, anayejali na muelewa na sio wale watakaonirudisha nyuma," amesema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO KUONDOKA**
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, anatazamia kuondoka Manchester United, huku Roma ya kocha Jose Mourinho na Sporting Lisbon zikivutiwa naye. ***(La Repubblica)***

**JESUS AKARIBIA ARSENAL**
ARSENAL wana "matumaini makubwa" ya kumsajili fowadi wa Manchester City, Mbrazil Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25. Washikabunduki hao wanatarajia pauni milioni 30 zitatosha, lakini City wanataka pauni milioni 50**. *(Sky Sports)***

**TIELEMANS SAFI**
ARSENAL bado wanaweza kumsajili kiungo wa Leicester, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, licha ya kuwa wanatarajiwa kukamilisha dili la kiungo mwingine wa Porto, Fabio Vieira mwenye umri wa miaka 22, ambaye ni Mreno. ***(Evening Standard)***

**TUCHEL NA LEWANDOWSKI**
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel angependa kumsajili mshambuliaji wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 33, Poland Robert Lewandowski, kuchukua nafasi ya Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29 - ambaye analengwa na Inter Milan. ***(ESPN)***

**SPENCE AWINDWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur ipo mstari wa mbele kumsajili mlinzi wa Middlesbrough, Djed Spence mwenye umri wa miaka 21, huku Nottingham Forest ikikubali kuwa huenda asijiunge nao, baada ya kukaa kwa mkopo City Ground msimu uliopita. ***(Northern Echo)***

**MAN NA DE JONG**
KLABU ya Manchester United ina imani Barcelona itapunguza bei yao ya pauni milioni 80 ili kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Guardian)***

**VLASIC KUTOLEWA**
WEST Ham ipo tayari kumtoa kwa mkopo mshambuliaji wa Croatia, Nikola Vlasic mwenye umri wa miaka 24, huku klabu za Hadjuk Split na Torino zikimtaka. ***(Dalmatinskiportal)***

**MORELOS ATAKIWA SEVILLA**
KLABU ya Sevilla ipo tayari kutoa pauni milioni 6.9 kwa mshambuliaji wa Rangers na Colombia, Alfredo Morelos mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes)***

**SOLOMON AWANIWA**
FULHAM iko tayari kukamilisha usajili wa pauni milioni 7 wa mshambuliaji wa Israel, Manor Solomon mwenye umri wa miaka 22, kutoka Shakhtar Donetsk. ***(Sun)***

**DENNIS NA EVERTON**
MSHAMBULIAJI wa Watford wa Nigeria, Emmanuel Dennis mwenye umri wa miaka 24, yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa na Everton msimu huu ikiwa fowadi wao wa Brazil Richarlison mwenye miaka 25, ataondoka. ***(Mail)***

**NIAKHATE KUUZWA**
KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kumnunua mlinzi wa Mainz, Mfaransa Moussa Niakhate mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MANE SASA RASMI MALI YA BAYERN

●●●Liverpool wakubali kumuuza kwa euro milioni 41, atajwa kwenda kuchukua mikoba ya Lewandowski kama..

**MUNICH, Ujerumani**

LIVERPOOL wamekubali ada ya euro milioni 41 kumuuza Sadio Mane kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich.

Wekundu hao watapata kwanza euro milioni 32 na nyongeza ya euro milioni 6 kulingana na idadi ya mechi itakazocheza na euro milioni 3 kulingana na mafanikio binafsi ya mchezaji mwenyewe na timu.

Liverpool walikataa ofa mbili kutoka kwa Bayern kabla ya klabu hizo mbili kukubaliana kuhusu kuuzwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Senegal, ambaye mkataba wake na wekundu hao ulikuwa unamalizika msimu ujao wa joto.

Alijiunga na Liverpool kwa pauni milioni 31 pamoja na pauni milioni 2.5 kama nyongeza kutoka Southampton mwaka 2016.

Tangu wakati huo, Mane alifunga mabao 90 ya Ligi Kuu England akiwa na klabu hiyo ya Anfield na kumaliza msimu uliopita akiwa na mabao 23 katika michuano yote.

Habari za kuondoka kwake zinafuatia usajili wa wiki iliyopita wa fowadi wa Uruguay, Darwin Nunez kutoka Benfica kwa dau la awali la pauni milioni 64.

Pamoja na washambuliaji wenzake Mohamed Salah na Roberto Firmino, ambao wote wana umri wa miaka 30, Mane amekuwa muhimu kwa mafanikio ya Liverpool katika miaka ya hivi karibuni.

Watatu hao waliisaidia klabu hiyo kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 na kisha kumaliza kipindi cha miaka 30 cha kusubiri taji la ligi katika msimu uliofuata.

Huu pia umekuwa mwaka wa kipekee kwa Mane, ambaye alishinda Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa na Senegal kabla ya kuisaidia Liverpool kushinda Kombe la Carabao na lile la FA na kumaliza washindi wa pili wa Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mane anatarajiwa kuchukua nafasi ya Robert Lewandowski pale Bayern, huku mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Poland akihusishwa na kuhamia kwa miamba wa Hispania, Barcelona.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
AL AHLY CAIRO
VERSUS
ZAMALEK
1 | 1.94
X | 3.16
2 | 4.11

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LEWANDOWSKI AIKATAA CHELSEA, KUTUA BARCA



**LONDON, England**

ROBERT Lewandowski amekataa nafasi ya kujiunga na Chelsea msimu huu wa joto huku mshambuliaji huyo wa Bayern Munich akilenga kutaka kutua Barcelona.

Akikataa kusaini mkataba mpya huku akiwa amebakisha mwaka mmoja tu katika mkataba wake wa sasa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na amezivutia klabu nyingi ikiwemo Chelsea.

Ikiwa ni kwa mara ya kwanza ikiripotiwa na Sport, Lewandowski amekataa nafasi ya kujiunga na kikosi hicho cha Ligi Kuu England, badala yake anataka kwenda Barcelona.

Thomas Tuchel anataka kuleta mshambuliaji wa ubora wa juu pale Stamford Bridge baada ya Romelu Lukaku kutokuwa na kiwango bora tangu arejea hapo na kocha huyo anamuaona nahodha huyo wa Poland kuwa anafaa kujiunga na Chelsea.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 anaonekana kuvutiwa zaidi na Barcelona huku kocha Xavi akisemekana kuwa Lewandowski ndio mlengwa wake mkuu wa uhamisho.

Nia ya awali ya Chelsea kumnunua mshambuliaji huyo ilichochewa na ugumu wa Barcelona kusajili wachezaji wapya kutokana na matatizo yao ya kifedha.


Lakini baada ya klabu hiyo ya LaLiga kupata udhamini wa Spotify sasa wana uwezekano wa kukamilisha usajili wa Lewandowski.

Paris St Germain pia walidaiwa kutaka kupata huduma ya mshambuliaji huyo kwa msimu huu wa joto.

Lewandowski anatarajiwa kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Hispania siku chache zijazo.

Atajiunga na mshambuliaji wa zamani wa Borussia Dortmund na Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang katika miamba hiyo ya Hispania baada ya kukaa kwa miaka 12 akicheza nchini Ujerumani.

# De Jong huyo Man United



**MANCHESTER, England**

KIUNGO Frenki de Jong anaonekana sasa safari ya kujiunga na Manchester United imekaribia baada ya kuripotiwa 'kusafisha kabati lake' kule Barcelona.

Kiungo huyo amekuwa akiwaniwa na Man United katika miezi ya hivi karibuni wakitaka akazibe pengo la Paul Pogba anayeondoka.

De Jong amewahi kufanya kazi na kocha mpya wa Man United, Erik Ten Hag kule Ajax. Walishinda mataji mawili ya nyumbani na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja mwaka wa 2019 ambapo walitolewa na Tottenham Hotspur.

Kwa mujibu wa AS, Barca 'wameongeza mawasiliano' na klabu zinaovutiwa huku wakitafuta kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi kwa pauni milioni 80, ikiwa ni zaidi ya pauni milioni 20 ambazo United wametoa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa mchezaji muhimu katika klabu hiyo kwa miaka mitatu iliyopita, akicheza michezo 140 katika michuano yote na kufunga mabao 13.

Kumuuza de Jong kunaweza kuwa hatua nzuri kwa klabu kwani wametatizwa na masuala ya fedha ya hivi majuzi.

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# KOCHA APONGEZA WACHEZAJI KUTWAA ZFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa timu ya Kipanga, Hassan Abdallah amefurahi kutimiza lengo lake la kutwaa ubingwa wa kombe la ZFF (FA Cup) na kuwapa pongezi nyingi wachezaji na viongozi wa timu hiyo.

Kipanga ambayo ni timu ya Jeshi ilitwaa ubingwa huo Ijumaa baada ya kuifunga Chipukizi bao 1-0.

Bao hilo pekee kwenye mchezo huo, lilifungwa na mchezaji, Mundhiri Abdallah Vuai katika dakika ya 36.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Abdallah alisema pongezi za pekee zinastahili kwa wachezaji na viongozi wote wa timu hiyo kwa jitahidi kubwa walizofanya na kuweza kutwaa Kombe hilo.

Alisema timu hiyo tangu awali ilijikita katika kutafuta Kombe la FA baada ya kupoteza matumaini katika Ubingwa wa ligi Kuu ya Zanzibar.

Mchezo huo uliochezwa katika uwanja wa Amaan majira ya saa 10:00 Alasiri ulihudhuriwa na mgeni rasmi Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo, Ali Abdulgulam.

Timu ya Kipanga mbali na kukabidhiwa Kombe pia imepokea mfano wa Hundi ya kitita cha Shilingi milioni 30, wakati timu ya Chipukizi imepokea hundi ya kitita cha Shilingi milioni tano.

Wakati huo huo, leo timu ya KMKM inatarajia kukabidhiwa Kombe lao la Ubingwa wa ligi kuu ya Zanzibar msimu huu mara baada ya mchezo wao wa mwisho ligi hiyo dhidi ya Mlandege.

KMKM atakabidhiwa hilo pamoja na kitita cha Shilingi milioni 50 kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.



Wanamuziki wa Bendi ya Tunaweza ya Watu wenye Ulemavu, ikitumbuiza wakati wa maadhimisho ya Mtoto Mwenye Ulemavu kuelekea kilele cha maadhimisho ya Mtoto wa Afrika Juni 16 jijini Dar es Salaam juzi, iliyoambatana na harambee yakuwachangia watoto wenye ulemavu ili kupatiwa huduma ya Bima ya Afya iliyoongozwa na Waziri Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 19 waunda timu ya riadha Tanga

**Na Cheji Bakari,Tanga**

CHAMA cha Riadha mkoa wa Tanga kimesema kuwa tayari kimeunda timu ya riadha ya mkoa ambapo kuna jumla ya wachezaji 19.

Akizungumza na Nipashe Jumapili Mwenyekiti wa chama hicho, Sofia Wakati amesema kuwa wachezaji hao ni wanawake na wanaume ambapo idadi yao ipo sawa kwa jinsia zote.

Amesema kuwa wachezaji hao wametoka katika wilaya zote za mkoa wa Tanga.

"Riadha mkoa wa Tanga tayari tumeunda timu ya riadha ya mkoa ambapo kuna jumla ya wachezaji 19 ambapo idadi yao ipo sawa kati ya wanawake na wanaume," alisema.

Amesema kuwa timu hiyo ilikuwa iende Dar es Salaam kwa ajili ya mashindano ya Taifa ya riadha Juni 23 hadi 25 lakini mashindano hayo yamesogezwa mbele kupisha uchaguzi mdogo wa Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa Chama cha Riadha Taifa.(RT).


SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 19/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4295 | OLS Oulu vs JJK Jyvaskyla | 4.91 | 4.32 | 1.50 |
| 14:00 | 4606 | Busan I Park vs Gyeongnam | 3.29 | 3.43 | 1.98 |
| 14:30 | 4514 | Tammeka Tartu vs Tallinna JK Legion | 1.86 | 3.64 | 3.49 |
| 15:00 | 1113 | Eskilsminne IF vs Torslanda IK | 1.25 | 5.67 | 8.02 |
| 15:00 | 2149 | Osterlen FF vs Nosaby IF | 1.28 | 5.30 | 7.85 |
| 15:00 | 4100 | Zalgiris Kaunas vs Lietava Jonava | 1.03 | 9.79 | 39.18 |
| 16:00 | 1183 | Uzbekistan U23 vs Saudi Arabia U23 | 2.32 | 2.74 | 3.28 |
| 16:00 | 1483 | Torque vs CA Rentistas | 1.71 | 3.53 | 4.32 |
| 16:00 | 2879 | Selangor FC vs Sarawak | 1.54 | 4.14 | 4.83 |
| 16:00 | 3078 | Kedah vs Johor Darul Takzim | 5.10 | 4.12 | 1.51 |
| 16:00 | 3564 | IK Start vs Stabaek | 2.14 | 3.34 | 3.00 |
| 16:00 | 4471 | FK Arsenal Dzerzhinsk vs Shakhter Soligorsk | 9.81 | 5.30 | 1.24 |
| 16:00 | 5403 | IFK Haninge vs Tegs SK | 1.21 | 5.72 | 9.87 |
| 16:00 | 5561 | Stjordals vs Blink-Brann | 6.68 | 5.11 | 1.33 |
| 17:00 | 2180 | Nordvarmland FF vs Karlslunds IF | 2.66 | 3.69 | 2.21 |
| 17:00 | 2955 | Raagsveds IF vs Sandvikens AIK FK | 1.52 | 4.50 | 5.00 |
| 17:00 | 3434 | San Martin SJ vs Ferro CO | 1.95 | 3.05 | 3.88 |
| 17:00 | 3749 | Tiller IL vs Junkeren | 5.80 | 5.80 | 1.36 |
| 17:00 | 5000 | Mirassol SP vs SAO Jose RS | 1.81 | 3.29 | 4.12 |
| 17:00 | 5444 | Guarani SP vs CSA AL | 2.32 | 2.89 | 3.09 |
| 17:15 | 2322 | Flora Tallinn vs Nomme Kalju | 1.49 | 3.93 | 5.70 |
| 18:00 | 4343 | Gomel vs Dinamo Brest | 1.57 | 3.63 | 5.30 |
| 18:00 | 5472 | Nardo vs Rana FK | 1.70 | 4.23 | 3.64 |
| 18:00 | 5653 | FK Panevezys vs Zalgiris | 3.19 | 3.14 | 2.14 |
| 18:30 | 1982 | KuPS Akatemia vs FC Lapa | 1.20 | 6.30 | 9.25 |
| 18:30 | 1989 | Serbia U19 vs Israel U19 | 1.91 | 3.42 | 3.52 |
| 18:30 | 5390 | Ilves 2 vs FC Honka/Akatemia | 2.46 | 3.74 | 2.34 |
| 18:30 | 5661 | GBK Kokkola vs Komeetat | 1.58 | 4.30 | 4.60 |
| 19:00 | 1243 | Tromso vs Haugesund | 1.66 | 3.82 | 4.73 |
| 19:00 | 1862 | Viking vs Sandefjord | 1.28 | 5.62 | 8.84 |
| 19:00 | 2742 | Jerv vs Ham-Kam | 2.92 | 3.27 | 2.34 |
| 19:00 | 3524 | Lillestrom vs Rosenborg | 2.07 | 3.38 | 3.38 |
| 19:00 | 4522 | Odd Ballklubb vs Molde | 3.57 | 3.62 | 1.93 |
| 19:00 | 5743 | CA Tigre vs Banfield | 1.99 | 3.00 | 3.79 |
| 19:30 | 3428 | Melipilla vs Coquimbo | 2.51 | 3.30 | 2.51 |
| 19:45 | 2987 | San Telmo vs Quilmes | 3.18 | 3.08 | 2.17 |
| 20:00 | 1330 | Slavia Mozyr vs FC Minsk | 2.80 | 3.14 | 2.36 |
| 20:00 | 5131 | CS Cartagines vs CS Herediano | 2.56 | 3.30 | 2.46 |
| 21:00 | 2528 | Gimnasia Jujuy vs Temperley | 2.21 | 2.80 | 3.44 |
| 21:00 | 3091 | Al Ahly Cairo vs Zamalek | 1.94 | 3.16 | 4.11 |
| 21:00 | 5319 | HFX Wanderers FC vs Forge FC | 3.47 | 3.47 | 1.91 |
| 21:00 | 5400 | Atletico Grau vs Sporting Cristal | 3.83 | 3.49 | 1.81 |
| 21:00 | 5496 | Aalesunds vs Valerenga | 2.42 | 3.33 | 2.77 |
| 21:00 | 5631 | England U19 vs Austria U19 | 1.57 | 4.13 | 4.52 |
| 21:30 | 4666 | Huracan vs Atletico Tucuman | 1.83 | 3.34 | 3.93 |
| 22:00 | 2909 | Corinthians vs Goias | 1.56 | 3.44 | 5.90 |
| 22:00 | 3277 | Coritiba vs Atletico Pr | 2.43 | 3.00 | 2.81 |
| 22:00 | 4837 | Tenerife vs Girona | 2.34 | 2.90 | 3.25 |
| 22:00 | 4901 | Atletico Mineiro vs Flamengo | 2.09 | 3.24 | 3.19 |
| 23:30 | 2004 | Deportivo Maldonado vs CA Penarol | 3.91 | 3.18 | 1.89 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumapili Juni 19, 2022

Nipashe



## Mane sasa rasmi mali ya Bayern

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo wa leo wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya KMC utakaopigwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA KUANIKA MAJEMBE YOTE

●●● Wapo nyota kutoka Ghana, Nigeria na DR Congo, pia itaweka hadharani majina ya wachezaji wanaowatema...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema siku yoyote kuanzia kesho Jumatatu itaanza kutangaza baadhi ya wachezaji wapya ambao imewasajili kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema mbali na kuanza kuwatangaza baadhi ya wachezaji wao wapya, lakini watakuwa wakitumia fursa hiyo kutangaza wachezaji ambao itawaacha.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juu ya mipango mbalimbali ya klabu, ikiwemo usajili, Ahmed amesema hadi sasa bado wanaendelea kuzungumza na kuwasainisha baadhi ya wachezaji bora kabisa barani Afrika.

"Kila mchezaji mzuri hapa Afrika ambaye anafahamika na mashabiki wengi tumejaribu kuzungumza nao kwa sababu tupo kwenye maboresho makubwa kwenye kikosi chetu, dhamira ni kuwakusanya wachezaji hao bora na kuwaleta klabu ya Simba," alisema.

"Nikuambie tu tunaendelea kuzungumza nao na kuwasainisha baadhi, muda si mrefu, kuanzia kesho tutawatangaza wachezaji ambao tumeshaafikiana nao makubaliano, lakini pia tutaweka hadharani majina ya wachezaji ambao tutaachana nao," aliongeza.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kuwa watulivu na kuepukana na propaganda zinazoenezwa kuhusu timu yao.

"Wanachama na mashabiki wa Simba wawe watulivu, wasiwe na papara, mashaka, wala hofu hata kidogo na viongozi wao tunafanya usajili makini na bora, tunafahamu tumeangukia wapi, wapi panavuja, tunakwenda kuboresha maeneo yote hayo, hatuleti mtu au wachezaji ambao wakifika hapa unaanza kujiuliza, huyu alikaaje misimu mitatu akiwa amefunga mabao mawili tu, tunaleta wachezaji wenye rekodi nzuri ili waje kufanya kazi."

Tayari klabu ya Simba imemtangaza rasmi straika hatari, Moses Phiri akitokea Zanaco ya Zambia, huku pia kukiwa na habari ya kusajili baadhi ya nyota mbalimbali barani Afrika.

Pia mtandao wa Ghana Soccernet umeripoti kuwa Simba iko kwenye hatua za mwisho kumnasa winga na kiungo mshambuliaji wa Klabu ya Bechem United, Augustine Okrah mwenye umri wa miaka 28, ambaye amefunga mabao 14 kwenye mechi 31 za Ligi Kuu msimu huu.

Taarifa zinasema kuwa atasaini mkataba wa miaka miwili au mitatu kuitumikia Simba na hivi karibuni atasafiri kutoka Ghana kuja Tanzania kwa ajili ya mazungumzo ya mwisho na vipimo vya afya.

Wachezaji wengine ambao tetesi zinasema huenda wakavaa uzi mwekundu msimu ujao ni Morlaye Sylla raia wa Guinea, anayeichezea klabu ya Horoya kutoka nchini humo na Cesar Manzoki, Mkongomani mwenye uraia wa Afrika ya Kati, anayeichezea Vipers ya Uganda na mshindi wa kiatu cha dhahabu msimu uliomalizika.

Wengine ni Vicent Akapan, Mnigeria anayeichezea Coastal Union, akiwemo pia Abdul Selemani 'Sopu', pia wa Coastal, winga ambaye ametokea kwenye kikosi cha pili cha Simba, akaenda kucheza kwa mkopo Ndanda FC, kabla ya kuibukia kwenye timu hiyo ya Tanga.

## Nabi ataka straika mwingine Yanga SC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Yanga, Nesredine Nabi amesema bado anahitaji mshambuliaji mwingine wa mabao kwa akili ya kuimarisha zaidi safu ya ushambuliaji kwa msimu ujao wa mashindano.

Hadi sasa Yanga imemalizana na mshambuliaji mmoja ambaye ni Lazarous Kambole na Stephan Aziz KI ambaye bado klabu hiyo haijathibitisha kumsajili nyota huyo kutoka nchini Burkina Faso.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema uongozi unatakiwa kuwa makini kutumia kipindi cha usajili kwa kutofanya makosa na kufuata mapendekezo, na anahitaji kuongezewa mshambuliaji mwingine mbali na wawili ambao amepewa majina yao.

Alisema wamefanikiwa kumsajili Kambole, amehakikishiwa na mabosi wake kwamba wako katika mchakato wa kupata saini ya Aziz KI, lakini bado anataka mshambuliaji mwingine kwa ajili ya kuimarisha zaidi kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya michuano ya kimataifa.

"Tukiachana na wale nilioambiwa nafikiria kuongeza mshambuliaji mwingine bora zaidi mbali na hao wawili ambao watakuja kusaidiana na Fiston Mayele," alisema Nabi.

"Nimeambiwa wachezaji wawili tutakuwa nao msimu ujao ni Kambole na Aziz Ki, ni wachezaji wazuri, lakini kulingana na msimu ujao wa mashindano tunahitaji kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji kuwa na mtu mwingine kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu."

Alisema anahitaji mshambuliaji mwingine mwenye uwezo mkubwa na bora, hahitaji kuyumba katika usajili wa msimu ujao kwa ajili ya kwenda kufanya ushindani mkubwa na kufanya kwao vizuri katika mashindano yajayo lazima wawe na watu watatu ili kutokuwa na mashaka.

"Tutakapokuwa na timu bora ya mashindano ya kwenye mashindano ya CAF moja kwa moja tutakuwa na timu nzuri, huku ndani kitu kizuri zaidi ndoto zangu pia hazitofautiani na uongozi wa klabu hii, sote tunaitakia mafanikio makubwa msimu ujao," alisema Nabi.

Mwisho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >